VUNJA UKIMYA

Sauti za Manusura wa Ukatili wa Kijinsia na Kingono
Shuhuda za Kweli kutoka kwa Wanawake na Wasichana ndani ya Tanzania



"Sehemu ngumu zaidi haikuwa ukatili wenyewe-bali kuambiwa ninyamaze."

WOMEN ACTION TOWARDS ECONOMIC DEVELOPMENT (WATED)

Kigamboni and Kisarawe kola village,
P.O. Box 3710, Dar es Salaam,
Tanzania

+255 745 950 950
info@wated.or.tz
www.wated.or.tz

USHAURI KUHUSU MAUDHUI

Kitabu hiki kina maudhui kuhusu ukatili wa kingono, unyanyasaji na unyonyaji.

Baadhi ya simulizi zilizopo katika kurasa hizi zinaweza kuwa ngumu kuzisoma au kuamsha hisia kali za kuumiza kwa baadhi ya wasomaji. Tafadhali zingatia usalama na ustawi wako unapokisoma kitabu hiki. Unaweza kupumzika, kutafuta msaada wa kitaalamu, au kuacha kusoma ikiwa maudhui yatakuwa magumu kwako.

UJUMBE WA MAADILI NA ULINZI WA MANUSURA

Ushuhuda wote uliopo katika kitabu hiki ni wa kweli. Majina yaliyotumika sio “majina halisi”, maeneo yameelezwa kwa ujumla, na baadhi ya taarifa zinazoweza kuwatambulisha wahusika zimebadilishwa ili kuwalinda manusura.

Simulizi zimewasilishwa kwa ridhaa kamili ya waliohusika na bila kubadilisha maana yake.

Lengo la kitabu hiki ni kurekodi ushuhuda, kuongeza uelewa, na kufanya utetezi - si kuleta msisimko au kufanya tukio lionekane la kuvutia kupita kiasi.

SABABU ZA KUWAPO KWA KITABU HIKI

Kitabu hiki kipo kwa sababu simulizi nyingi za ukatili wa kijinsia na kingono hazisikiki, haziaminiki, au haziandikwi kwa namna inayoheshimu maisha ya waliopitia matukio hayo. Mara nyingi sauti za manusura huchujwa, kufupishwa, kulainishwa au kubadilishwa ili ziendane na ripoti, takwimu au habari zilizoko kwenye chati. Kwa kufanya hivyo, ukweli wa matukio waliyoyapitia hupotea.

“VUNJA UKIMYA”, iliandaliwa kufanya jambo tofauti.

Dhamira ya kitabu hiki ni rahisi na ya makusudi: kusikiliza na kuchukua hatua ili kutokomeza ukatili.

Hadithi utakazosoma zimeelezwa kwa sauti za manusura wenyewe, kama walivyozisimulia. Hazijaandikwa upya ili zionekane za kusisimua, za kutia moyo, au rahisi kusomeka. Pia hazijahariri wa ili kulinda mifumo, taasisi au faraja ya kijamii. Mabadiliko yaliyofanywa ni yale tu ya kulinda utambulisho wa wahusika, si kubadilisha maana ya simulizi.

Hadithi hizi hazikuandika upya.
Tulizisikiliza.

Kwa kuweka sauti za manusura katikati, kitabu hiki kinapinga hukumu, lawama na kurahisisha mambo. Hakimwombi msomaji aamue nani yuko sahihi au nani si sahihi. Kinamwomba msomaji ashuhudie, akae na hisia zisizopendeza, na atambue madhara kwa binadamu yanayotokana na ukimya, mamlaka, na uzembe.

Kitabu hiki hakilengi kukushtua.
Kinalenga ukweli.

JINSI YA KUSOMA KITABU HIKI

Hiki si kitabu cha kukisoma kwa haraka.

Soma polepole.
Pumzika unapohitaji.
Rudi kukisoma pale utakapokuwa tayari.

Baadhi ya hadithi zinaweza kuonekana za kawaida kwako. Nyingine zinaweza kuwa ngumu sana kuzisoma. Usiruke hadithi kwa sababu tu inaumiza. Mara nyingi, kwenye maumivu ya hisia ndiko uelewa unakoanzia.

Hadithi hizi si takwimu.
Si tafiti za kujifunzia.
Si mafunzo yaliyofungwa kwenye hitimisho.

Kila hadithi inasimama yenyewe, ikiwa imeundwa na maisha halisi, mazingira maalumu, na wakati fulani katika maisha ya mhusika. Hakuna namna moja ya kukabiliana na ukatili, au ya kuendelea na maisha, na wala hakuna njia sahihi ya kushahimilivu madhara baada ya kupitia ukatili.

Kwa watunga sera, wataalamu na viongozi: sikilizeni kabla ya kujibu, na mjibu bila kuhukumu.

Kwa wanajamii na wasomaji wengine: epukeni kuhukumu au kulinganisha. Hadithi hizi haziombi idhini, zinaomba kusikilizwa.

Ikiwa kitabu hiki kitaibua hisia au kumbukumbu zinazoumiza, jipe muda wa kupumzika. Kuacha kusoma kwa muda si udhaifu - ni kujitambua.

Kitabu hiki hakikuombi urekebishe kila kitu.
Kinakuomba usigeuze macho upande mwingine.

MILA ZINAZOFICHA UKATILI WA KIJINSIA

- Angel (Jina sio halisi)
- Nina miaka 71
- Nilisoma mpaka kidato cha nne
- Ninaishi Tanga. Ninafanya kazi kama Mjasiliamali

Niliwahi kuolewa, lakini baadaye nikaachika. Mimi ni mama mwenye watoto kumi na mbili, ingawa watoto wanne walifariki dunia. Ili kuendesha maisha yangu, nafanya shughuli mbalimbali kama kufua, kulima na kufyeka. Pamoja na kazi hizo, ukiniona nipo maridadi na muonekano wangu uko vizuri. Nyumbani ninaishi na mtoto mmoja, wakati mtoto mwingine yuko Muhimbili kwa ajili ya matibabu akiwa anasaidiwa na dada zake wanaoishi Dar es Salaam. Pia nina wajukuu ninaowasomesha, kwa sababu baba yao alifariki dunia. Kwa uwezo wangu mdogo, kila siku natoa shilingi 3,000 kwa ajili ya wajukuu wangu kwenda shule.

Mnamo mwaka 1989, baada ya kuachika na mume wa kwanza, niliolewa tena. Lakini aliyenioa sikukaa naye sana, alifariki dunia. Kwa sisi Waislamu, unapofiwa na mume unakaa eda, ambacho ni kipindi cha kuomboleza. Baada ya hapo nilielezwa kuwa nilitakiwa kurithiwa. Mimi nilikataa. Lakini nikaambiwa kuwa kwa mujibu wa mila na desturi, ni lazima mwanamke arithiwe, vinginevyo anaweza kupata matatizo makubwa ya kiafya yanayoitwa "Kitigo" ambayo yanaweza kuzuilika kupitia utakaso wa wajane.

Nilipoendelea kuuliza kuhusu Kitigo, nikaambiwa kuwa ni ugonjwa anaoupata mwanamke anayekataa kurithiwa, ambapo anaweza kupooza mgongo au kiuno na kushindwa kutembea. Wakanieleza pia namna Kitigo kinavyotolewa kupitia utakaso wa wajane. Hutafutwa mwanaume mwingine ambaye haumjui na yeye hakujui.

Mwanaume huyo analipwa, na vitenge viwili hununuliwa. Vitenge hivyo hupelekwa porini, na wewe unatangulia kwenda huko. Unavaa kitenge kimoja, kingine kinatandikwa chini. Halafu unasubiri huyo mwanaume aje ili mkutane kimwili. Tukio hilo linafanyika gizani kiasi kwamba humuoni anayekuja kukuingilia. Mkishamaliza, kila mtu anaondoka na kushika njia yake.

Pia waliniambia kuwa huo ni utando au mnyororo, na kwamba usipotoa Kitigo, hata ukifa yeyote atakayechukua nguo zako anaweza kupata matatizo hayo. Hivyo watoto wako hawatarithi mali zako. Hata kama una masanduku kumi ya nguo, yote yanaweza kuchomwa moto au kutupwa.

Kutokana na mazingira hayo, nilijikuta sina nguvu ya kukataa tena. Nilikuwa tayari nimekataa kurithiwa, na sasa nilikuwa nawekewa shinikizo kwamba familia ingeharibika, mikosi ingetokea, na hata watoto wangu wasingeweza kurithi mali zangu. Kwa hiyo, ilibidi nikubali kufanyiwa utakaso wa wajane unaoondoa Kitigo.

Baada ya hapo nikarudi na kuendelea na maisha yangu. Nilimaliza siku 40 za kuomboleza. Nilijaribu kuendelea na shughuli zangu za kawaida za kujitafutia riziki, lakini baada ya miezi kama sita nilianza kuona hali yangu inabadilika.

Uzito ulianza kupungua, nilianza kukohoa, nilikuwa napatwa na homa mara kwa mara na nguvu zikaanza kuniishia. Sikuelewa shida ilikuwa ni nini.

Katika watoto wangu, nilimuamini binti yangu mmoja kunitunzia siri. Nikamweleza jinsi nilivyokuwa najisikia pamoja na kila kitu kilichokuwa kimetokea. Baada ya kunisikiliza, akaniambia, "mama, usijali." Asubuhi yake tukaondoka pamoja kwenda hospitali. Nilipofika nikawaambia kwamba nimekuja kuangalia afya yangu kwa sababu nina homa za mara kwa mara, uzito unapungua na nguvu zinaniishia.

Nilipimwa Virusi Vya UKIMWI (VVU). Kisha wakaniuliza, "Mama, ukiambiwa huna maambukizi, utafanya nini?" Nikasema, "nitamshukuru Mungu." Halafu wakaniuliza tena, "na ukiambiwa una maambukizi?" Pale nilisita kidogo. Mtoto wangu akaniambia, "mama jibu." Nikasema, "pia nitamshukuru Mungu. Labda ndio andiko langu, na kama kuna dawa za kutumia, nitatumia."

Waliniambia nitoke nje kwanza. Nilipotoka nje nilikuwa kama nimepagawa. Nilikuwa natembea hospitalini bila kujua nifanye nini. Nikakutana na mwanaume mmoja akaniuliza, "Mama, una shida gani, mbona upo hivyo?" Wakati huo mwanangu akaja pale nilipo na kusema majibu yameonyesha nimeathirika. Tukarudi ndani, nikapewa ushauri nasaha. Walinipa moyo sana na kunihimiza nitumie dawa.

Nilipokuwa naendelea na matibabu, nilikaa kwa dada yangu ambaye tumezaliwa tumbo moja. Lakini huko nilikumbana na ukatili mwingine mkubwa wa kunyanyapaliwa. Katika suala la chakula, dada yangu alikuwa amenitenga kikombe changu, sahani yangu na chakula changu. Muda wa kula, chakula kiliwekwa kwenye sahani na kusukumwa kwa mti hadi kinifikie. Nilikuwa nalia sana kwa ile hali ya kunyanyapaliwa. Mwanangu akiwepo, ndiye aliambiwa aniletee chakula.

Wakati huo pia nilikuwa natumia mitishamba kwa sababu dawa za hospitali hazikupatikana kwa urahisi. Hata hivyo baadaye hali yangu ilizidi kuwa mbaya.Niliumwa sana na nikapelekwa mpaka wodi ya wagonjwa mahututi kwa sababu kinga zilishuka sana. Ndipo nilipoanzishiwa dawa za ARV baada ya kuanza kupatikana.

Tangu wakati huo nimeendelea kutumia dawa mpaka leo, na naendelea vizuri sana. Hata ukiniangalia huwezi kujua nimepitia nini.

Hadi leo suala la utakaso wa wajane bado lipo katika maeneo mbalimbali ya Tanga kama Mombo, Lushoto, Bumbuli na Mlalo. Jamii nyingi bado zinaendelea na mila hizi, na wanawake bado wanarithiwa au kufanyiwa utakaso wa wajane.

Baadaye familia yangu walipogundua kuwa nimeambukizwa VVU kutokana na kile walichonilazimisha kukifanya kule porini walijilaumu sana. Lakini athari yake tayari imeniumiza kisaikolojia. Hadi leo sijawahi kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanaume yeyote. Ninapowaona wanaume, mara nyingi nahisi kama wote ni wale wale wanaofanya ukatili.

Huu ni wito wangu kwa jamii na serikali: jambo hili lipigwe vita na likomeshwe kabisa.

UTAKASO WA WAJANE NI UKATILI WA KINGONO ULIOGEUZWA KUWA DESTURI, UOVU

Ni aina ya unyanyasaji ambao mara nyingi huwezi kuutolea taarifa popote, kwa sababu umehalalishwa na jamii na kufanywa kuwa siri ya familia. Lakini mwisho wa siri hiyo ni maumivu ya kudumu, yanayowaacha wanawake na athari kubwa za kiafya na kisaikolojia.

Ni lazima watu wapewe elimu ya namna ya kutoa taarifa za ukatili. Ingawa serikali na mashirika mbalimbali yameanza kupinga utamaduni huu, ukuta wa usiri bado ni mkubwa sana. Watu wanaogopa aibu, na aibu hiyo ndiyo inayozika ukweli na kuendeleza ukatili huu gizani.

NATAKA JAMII IJUE KUWA SI KILA KITU KINACHOITWA MILA NI SALAMA. KUNA MILAAMBAZO KIMSINGI NI UKATILI.

Ukatili huo ukivikwa kilemba cha desturi, madhara yake huwa makubwa na ya kutisha, kwa mwanamke, kwa watoto wake, na kwa jamii nzima.

NJIANI PEKE YANGU



- Merina (Sio jina halisi)
- Nina miaka 24
- Nilisoma mpaka kidato cha nne
- Ninaishi Dar es Salaam. Nafanya kazi za nyumbani

Nilizaliwa na kukulia mkoani Morogoro chini ya malezi ya wazazi wangu. Huko ndiko nilikosoma shule ya msingi na sekondari hadi kumaliza kidato cha nne. Maisha yangu ya utotoni na ujana wa mwanzo yalikuwa ya kawaida kama ya wasichana wengine, na mpaka sasa bado sijaolewa.

Katika maisha yangu pia niliwahi kupata changamoto ya kiafya. Uvimbe ulianza kwenye mkono wa kushoto na baadaye ukaanza kuhamia kwenye bega. Kutokana na hali hiyo nilianza kupata matatizo ya mkono na mguu. Wazazi wangu walihangaika sana kunipeleka hospitali mbalimbali kutafuta matibabu.

Nilifanyiwa vipimo vingi lakini ugonjwa haukuonekana wazi. Baadaye walijaribu pia kunipeleka kwa wataalamu wa tiba za asili. Baada ya matibabu kadhaa hali ilianza kupungua kidogo, lakini mpaka leo bado nina changamoto kwenye viungo vyangu, hasa mkono kugeuka na vidole ambavyo haviwezi kunyooka vizuri.

Nakumbuka ilikuwa mwaka 2020 kulikuwa na kijana mmoja ambaye alikuwa ananifuatilia sana. Alikuwa akijaribu kunishawishi ili niwe naye kimapenzi, lakini hakuwahi kufanikiwa kwa sababu nilikuwa nikimkataa mara zote.

Siku moja kulikuwa na shughuli kwa shangazi yangu, na alinialika niende. Niliaga wazazi wangu nyumbani kisha nikaenda kushiriki kwenye shughuli hiyo.

Shughuli ilienda vizuri mpaka usiku, na mimi nikawa tayari kuondoka. Ilipofika mida ya saa moja usiku, nilimuaga shangazi yangu nikisema narudi nyumbani. Kutoka nyumbani kwa shangazi hadi nyumbani kwetu kulikuwa na umbali mfupi tu, hivyo nilikuwa narudi peke yangu.

Njiani nikakutana na yule kijana ambaye alikuwa ananifuatilia. Tulikuwa wawili tu barabarani; yeye na mimi. Alianza kunisumbua na kunizuia nisipite. Ghafla alinivuta mkono kwa nguvu. Sikuwa na uwezo wa kupambana naye, wala hapakuwa na mtu yeyote wa kunisaidia mahali pale.

KUTOKANA NA HALI YANGU YA MWILI SIKUWEZA KUJITETEA. YULE KIJANA ALINIVUTA KWA NGUVU NA KUNIINGIZA PORINI KANDO YA ILE NJIA. HUKO NDIPO ALIPONIFANYIA UKATILI WA KINGONO NA KUNIINGILIA PAMOJA NA KINYUME NA MAUMBILE.

Baada ya kufanya kitendo hicho alikimbia na kuniacha pale. Nilijisitiri kadiri nilivyoweza kisha nikarudi nyumbani. Yule kijana hakuwa mwenyeji wa kijiji chetu. Nilikuwa nimeshawahi kusikia jina lake na kumuona mara chache, lakini sikuwahi kumtilia maanani wala kuifahamu sura yake vizuri.

Ilikuwa ni siku hiyo tu ndipo nilipoweza kuiona na kuikumbuka sura yake kwa uwazi. Nilipofika nyumbani niliwaeleza wazazi wangu kile kilichotokea. Wazazi wangu walichukua hatua mara moja na kwenda kutoa taarifa kwa polisi ili yule kijana ashughulikiwe kisheria. Baadaye tulisikia pia kutoka kwa watu wengine kwamba kijana huyo alikuwa na tabia ya kuwaharibu wasichana wa watu. Hata hivyo sikuwahi kufikiria kwamba siku moja ningekutana naye katika mazingira ya kutisha kama yale.

Baada ya tukio hilo maisha yangu yalibadilika. Baadaye iligundulika kuwa nilipata ujauzito kutokana na tukio hilo. Mama yangu ndiye mtu wa kwanza niliyemweleza kuhusu ujauzito huo.

Niliona si vyema kuficha jambo kama hilo kwa wazazi wangu. Mama akazungumza na baba yangu. Baba yangu ni mtu anayeheshimika sana katika jamii yetu na pia ni shekhe mkubwa. Tukio lile lingeweza kumfedhehesha sana katika jamii. Lakini licha ya hayo wazazi wangu hawakunilaumu wala kuninyoshea kidole.

Badala yake waliamua kunisimamia na kunitetea. Wazazi wangu pamoja na polisi walijaribu kumtafuta yule kijana. Upelelezi ulifanyika lakini hawakufanikiwa kumpata.

Baada ya muda tulilazimika kusimamisha ufuatiliaji wa kesi hiyo. Kutokana na hali hiyo na mazingira ya kijijini, familia yetu iliamua kuhama na kuja kuishi Dar es Salaam.

Nilienda hospitali na nilipokelewa vizuri na wahudumu wa afya. Wakati huo nilifikiria kutoa ujauzito, lakini wazazi wangu walinishauri nisiutoe. Waliniambia huenda Mungu amekujalia mtoto huyo kwa sababu maalum.

Walinihakikishia kwamba wangemlea na kumhudumia mtoto huyo. Kwa msaada wao niliamua kuendelea na ujauzito. Hospitalini walinifanyia vipimo mbalimbali na ninamshukuru Mungu kwamba sikupatikana na maambukizi ya VVU.

Hadi leo ninashukuru sana wazazi wangu kwa kunisimamia katika kipindi kile kigumu. Wao ndio waliomlea mtoto wangu na bado wanaendelea kunisaidia. Kwa sasa bado nina ndoto ya kujitegemea.

Kule kijijini tuna shamba la baba yangu, na kilimo ninachokipenda zaidi ni cha nyanya. Changamoto kubwa kwangu ni kukosa mtaji wa mbegu, dawa za kilimo na mipira ya kumwagilia shamba. Ninaamini kama ningepata msaada wa vifaa hivyo ningeweza kulima na kujitegemea katika maisha yangu.

UJUMBE WANGU KWA WENGINE NI KWAMBA WASIKATE TAMAA WANAPOKUTANA NA UKATILI WA NAMNA HII. WANAPASWA KUPAMBANA NA KUTAFUTA MSAADA NA KUTOA TAARIFA MAPEMA ILI WAHUSIKA WAWEZE KUCHUKULIWA HATUA.

Kwa wazazi pia ni muhimu kusimamia na kulinda watoto wao. Watoto wanahitaji ulinzi na malezi bora ili wawe salama katika jamii.

Kwa wasichana wenzangu ni muhimu kuwa makini na kutafuta msaada haraka wanapokutana na hatari. Jamii pia inapaswa kuchukua jukumu la kulinda wasichana na wanawake dhidi ya vitendo vya ukatili. Mimi binafsi bado nina matumaini makubwa ya kuwa na maisha bora huko mbeleni, na ninatamani siku moja niweze kujitegemea kikamilifu kupitia shughuli za kilimo ninachokipenda.

AJIRA INAPOGEUKA MTEGO

- Janeth (Sio jina halisi)
- Nina miaka 30.
- Nilisoma mpaka darasa la sita.
- Nimetokea Dodoma. Ninafanya kazi za Ndani.

Nilikuwa mdogo sana nilipoanza kufanya kazi hivyo sikupata nafasi ya kuendelea na shule kwa sababu ya mazingira magumu ya nyumbani. Nilikuwa naingia darasa la sita nilipoacha masomo, nikaanza kutafuta kazi ili kumsaidia bibi yangu aliyenilea tangu utotoni.

Nikiwa na umri wa miaka kumi na miwili, kuna dada mmoja alinichukua nyumbani na kuniambia niende kufanya kazi za ndani mkoani Arusha. Nilikuwa mdogo sana na sikuwa najua mambo mengi kuhusu dunia, nje ya nilipokulia. Tulifika eneo lile na nilianza kufanya kazi za nyumbani kwa mama aliyekuwa akifanya kazi katika nashamba ya kahawa.

Kazi yangu ilikuwa kufanya kazi za kawaida za nyumbani. Watoto wa yule mama walikuwa wanasoma shule za bweni, hivyo mara nyingi nilikuwa nyumbani peke yangu.

Baada ya muda mdogo wake alihitimu masomo ya chuo na kuja kuishi hapo nyumbani kwa dada yake. Nilimchukulia kama kaka yangu kwa sababu nilikuwa mdogo na nilimpa heshima kama kaka wa nyumbani. Alikuwa na kawaida ya kuniita nimpelekee chai au kumwandalia chakula. Mimi nilikuwa nafanya kazi hizo kwa unyenyekevu na adabu kama mfanyakazi wa nyumbani.

Siku moja dada yake alisafiri kikazi akatuacha nyumbani mimi na mdogo wake. Siku ile nilimpelekea chai kama kawaida. Baada ya kunywa chai aliniambia, “njoo ukae hapa.” Mimi nikawa naogopa. Nikajiuliza kwa nini ananiitia nikae kwenye kochi. Lakini nikasema ngoja nimsikilize. Nilipokaa, alinyanyuka na kuja karibu nami. Akaanza kunishika huku akiniambia: “wewe ni msichana mzuri kweli.” Nilianza kuogopa sana. Nilikuwa najiuliza uzuri wangu ni nini, na kwa nini kaka ninayemheshimu ananishika hivyo.

GHAFLA ALINIVUTA KWA NGUVU, AKANIZIBA MDOMO NA KUNIINGIZA CHUMBANI KWAKE. HUKO NDIPO ALINIBAKA.

Wakati huo sikuwa najua chochote kuhusu mambo hayo. Niliona damu na nilikuwa na maumivu makali sana. Nilikuwa bado mdogo, hata siku zangu zilikuwa bado hazijaanza. Baada ya kunifanyia kitendo hicho aliniambia: “ole wako umwambie mtu yeyote, nitakuua.” Nilijikuta nalia tu. Nilihisi kama usichana wangu umeharibika kabisa. Hofu aliyoniwekea ilinifanya nishindwe kusema kwa mtu yeyote. Nilihofia hata nikimwambia dada yake nitaonekana kama muongo. Baada ya tukio hilo aliendelea kunifanyia vitendo hivyo tena na tena. Kila dada yake akiwa hayupo nyumbani alikuwa ananifanya kama mke wake ndani ya nyumba.

Dada yake alianza kuona nimebadilika. Alikuwa ananiuliza kwa nini nimekuwa mtu wa mawazo au kama nimekumbuka nyumbani.

Lakini mimi nilikuwa namwambia hapana kwa sababu nilikuwa naogopa kusema ukweli. Sikuwa na pesa yoyote kwasababu sikujua jinsi ya kuhifadhi. Nilikuwa natuma pesa zote kwa bibi yangu aliyenilea. Nilikaa pale kazini kwa miezi mitatu, na katika kipindi chote hicho aliendelea kunifanyia ukatili. Hatimaye nikapata ujasiri wa kumwambia dada yake. Nilimweleza kuwa mdogo wake alikuwa amenifanyia vitendo hivyo. Lakini yule dada hakuniamini. Alisema namzushia mdogo wake. Baada ya hapo niliomba wanipatie nauli nirudi nyumbani.

Niliporudi nyumbani bado sikuwa najua kuwa nimebeba ujauzito, kwa sababu hata siku zangu zilikuwa bado hazijaanza.

BAADA YA MUDA NDIPO ILIONEKANA KUWA NILIKUWA MJAMZITO. NILIKUWA NA MIAKA KUMI NA MIWILI, NA NILIJIFUNGUA NIKIWA NA MIAKA KUMI NA MITATU.

Hali hiyo ilinipa maumivu makubwa sana kwa sababu nilikuwa napenda kusoma. Mara nyingi nilikuwa nawaza kama ningepata mfadhili nirudi shule. Lakini narudije shule nikiwa tayari ni mjamzito?

Ujauzito ule ulikuwa mgumu sana. Wakati wa kujifungua nilipata shida kubwa, karibu nifanyiwe upasuaji kwa sababu njia iligoma kufunguka. Nilimwaga damu nyingi sana na nilikaa hospitali muda mrefu madaktari wakipambana kuokoa maisha yangu. Nakumbuka hata siku ya kujifungua nilijikuta karibu najifungua peke yangu. Manesi walikuwa wameondoka kwa muda na bibi yangu alikuwa nje. Nilijifungua pale nikiwa nalia mimi na Mungu wangu tu, kisha wakaja kukata kitovu.

Baada ya kujifungua maisha yalikuwa magumu sana. Nilikuwa bado mtoto lakini tayari mama. Nililazimika kufanya kazi ndogo ndogo ili kumlea mtoto wangu. Wakati mwingine nilienda kuchota maji kisimani au korongoni, au kuuza vitu sokoni. Nilikuwa namwacha mtoto kwa bibi yangu kisha nakimbia kufanya kazi na kurudi kumnyonyesha. Kwa sababu nilikuwa bado mdogo, watu wengine walikuwa wananidhulumu hata kwenye kazi ndogo ndogo nilizokuwa nafanya.

Kulikuwa pia na watu waliokuwa wakisema maneno mabaya, wakiniita malaya kwa sababu nilizaa nikiwa mdogo. Maneno hayo yaliniumiza sana, lakini ilinibidi kuvumilia na kuendelea kupambana na maisha yangu.

Baada ya tukio hilo nilianza kuwachukia wanaume. Wengine walikuwa wananitongoza hata waliponiona nanyonyesha mtoto wangu, lakini mimi niliwakataa.

Wao walikuwa wanasema naringa, lakini hawakujua maumivu niliyokuwa nayo. Mara nyingi nilikuwa nikiingia ndani na kulia peke yangu. Nilimwambia bibi yangu kuwa maisha yangu yameharibika. Mwanzoni bibi alinilaumu, lakini nilimweleza wazi kuwa nilibakwa. Baadaye alinielewa na kuniamini. Kwa kweli sikupata msaada mkubwa. Nilikuwa mimi na bibi yangu tukipambana na maisha.

Tukio hilo lilibadilisha kabisa mwelekeo wa maisha yangu. Nilikuwa nimeambiwa naenda kufanya kazi na labda kusaidiwa kwenda shule, lakini nilichoambulia ni ujauzito na maisha magumu. Hata hivyo maumivu hayo yamenifanya kuwa mwanaharakati dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Sipendi kuona mtu mwingine anaonewa kama nilivyofanyiwa mimi. Hata kama sikuweza kusoma sana, ninajitahidi kuwasaidia wengine wanaokutana na ukatili. Kwa mabinti wadogo ningependa kusema wasikubali kudanganywa kirahisi kwenda kufanya kazi mbali bila ulinzi au usimamizi. Mara nyingi sehemu hizo zinaweza kuwa na hatari nyingi kwa watoto wa kike.

NI MUHIMU MANUSURA WA UKATILI WA KIJINSIA KUPATA MSAADA NA HAKI WANAPOTOA TAARIFA ZA

Ninatamani kuona sauti za wanawake, wasichana na watoto zinasikilizwa zaidi ili matukio ya ukatili yapungue katika jamii.

USALAMA UNAPOKOSEKANA NYUMBANI



- Chioma (Sio jina halisi)
- Nina miaka 35.
- Nilisoma mpaka kidato cha pili.
- Ninaishi Dodoma. Ninafanya kazi za nyumbani.

Nilikuwa na umri wa miaka mitatu nilipoanza kuishi chini ya malezi ya bibi yangu. Mama yangu alikuwa anafanya kazi na mara nyingi alikuwa anarudi usiku sana, hivyo alishindwa kutulea muda wote. Ndiyo maana maisha yangu ya utotoni kwa asilimia kubwa niliishi kwa bibi.

Maisha na bibi hayakuwa rahisi kwangu. Alikuwa mkali sana na alinipiga mara kwa mara. Kadri matukio hayo yalivyoendelea, nilianza kuhisi kuwa bibi hanipendi na huenda siku moja angeniumiza zaidi. Ndipo nilipomwambia mama yangu kuwa sitaki kuendelea kuishi na bibi, na nilitamani kwenda kuishi naye.

Nyumbani kwa mama pia maisha hayakuwa rahisi. Kazi yake ilimfanya arudi nyumbani usiku sana na alikuwa anaishi peke yake. Ilikuwa vigumu kwake kuniacha nilale peke yangu wakati wa usiku akiwa kazini. Ndipo akaamua kunipeleka kwa jirani yake ili nikale na kisha nilale huko kila usiku mama alipokuwa kazini. Nyumbani kwa yule jirani nilikuwa nalala pamoja na wasichana wakubwa ambao walikuwa watoto wa mwenye nyumba.

SIKU MOJA NIKIWA NIMELALA, WALE WASICHANA WALIANZA KUNISHIKA SEHEMU ZANGU ZA SIRI. MIMI SIKUWA NAELEWA WALICHOKUWA WANAFANYA

Walinipa maneno ya kunituliza wakisema kuwa si kitu kibaya, ni mchezo tu. Lakini walianza kuniingiza vidole kwenye sehemu zangu za siri. Nilihisi maumivu makali sana. Nilipopiga kelele waliniambia ninyamaze kwa sababu hayo ndiyo yangekuwa maisha yangu. Baadaye hawakuishia kutumia vidole tu. Walianza kuniingizia vitu vya ukubwa tofauti. Walinifanyia vitendo hivyo kwa muda mrefu mpaka walipoona wanaweza kuanza kunipeleka kwa wanaume.

Kuna siku nilipokwenda kulala pale, nilikuta kuna mwanaume ndani ya nyumba. Wale wasichana walitoka na kuniacha na huyo mwanaume. Naye alinifanyia ukatili wa kingono. Kufikia hapo haikuwa tena kitu cha kushangaza kwangu, kwa sababu walikuwa tayari wameshanizoesha kwa muda mrefu kwenye manyanyaso hayo. Sikuwahi kumwambia mama yangu kilichokuwa kinaendelea.

Baada ya muda mama yangu alihama kwenye ile nyumba, na hapo ndipo nilipata nafuu kidogo. Baada ya kuhama, mama aliamua kuanza kufanya biashara yake binafsi ili aweze kutuhudumia watoto wake. Biashara aliyokuwa anafanya ilikuwa kuuza pombe za kienyeji haramu, jambo ambalo lilikuwa na changamoto nyingi. Kulikuwa na changamoto za kukamatwa na polisi, changamoto za wateja na pia manyanyaso kutoka kwa jamii.

Baadaye, baada ya kuona maisha yanakuwa magumu, mama aliamua kuolewa na mtu mzima ili aweze kumsaidia kututunza. Mwanzoni maisha yalianza kuwa mazuri kidogo. Kulikuwa na afueni nyumbani lakini baadaye
Nilipoona imezidi, nikamwambia mama yangu. Mama alimuita na kumuuliza kuhusu tabia hiyo. Lakini alijibu kuwa yeye asili ya ya kwao baba kumshika mtoto wake ni jambo la kawaida, na kwamba hakuwa na nia mbaya. Mama alimwambia kuwa sisi ni kama mabinti wa zake na hatupendi maisha ya namna hiyo.

YULE BABA WA KAMBO ALIANZA TABIA YA KUNISHIKA MAKALIO, KIUNO NA KIFUA. ILIKUWA HALI AMBAYO SIKUIPENDA

Nilipoona imezidi, nikamwambia mama yangu. Mama alimuita na kumuuliza kuhusu tabia hiyo. Lakini alijibu kuwa kwenye utamaduni wao baba kumshika mtoto wake ni jambo la kawaida, na kwamba hakuwa na nia mbaya. Mama alimwambia kuwa sisi ni kama mabinti zake na hatupendi maisha ya namna hiyo.

Baada ya kumwambia mama yangu ukweli, yule baba alikasirika sana. Tangu hapo akaanza kunitesa zaidi. Usiku alikuwa ananiamsha mara kwa mara akiniagiza nimletee sigara, nimletee kiberiti au nimletee kopo la mkojo. Wakati mwingine alikuwa anakaa na kukojoa mbele yangu huku akinionyesha maumbile yake. Alikuwa ananifanyia mambo ya ajabu sana.

Kwa wakati huo mama hakuwa tena upande wangu; alikuwa upande wa mume wake. Nilipochoka manyanyaso hayo, siku moja nilimkabili yule baba kwa maneno makali na kumwambia wazi kuwa ananitaka kimapenzi. Nikiwa na miaka kumi na nne niliamua kuondoka nyumbani kwa mama na kwenda kuishi kwa shangazi yangu.

Lakini hata huko sikuwa na maisha ya amani. Kwa shangazi yangu pia kulikuwa na manyanyaso. Nilivumilia kwa sababu nilitaka kuendelea na shule. Lakini baadaye shangazi alianza kuniuza kwa wanaume kwa kuchukua pesa kutoka kwao. Wanaume walikuwa wanakuja nyumbani na kumwambia wanataka mwanamke.

Shangazi alinilazimisha kuondoka nao hadi kwenye gesti, ambako nilifanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono. Ilikuwa kama biashara ambayo shangazi yangu aliifanya kwa kutumia maisha yangu, na alihakikisha mama hajui chochote kinachonitokea.

Maisha yaliendelea hivyo mpaka nilipokuwa kidato cha pili. Ndipo alipotokea kijana mmoja ambaye alinionesha kunijali na kunipenda. Nilihisi kuwa ndiye mtu wa kwanza kunionesha upendo wa kweli katika maisha yangu.

Niliingia kwenye mahusiano naye, na nikiwa na miaka kumi na tano nilipata ujauzito wa mtoto wangu wa kwanza. Baada ya hapo kijana huyo akanikimbia, na nikapitia manyanyaso makubwa zaidi kutoka kwa shangazi ikabidi nitoroke na kwenda mitaani. Kulikuwa na kijana mwingine ambaye alikuwa ananitaka kwa muda mrefu, ikabidi nimkubalie na kwenda kuishi kwake. Lakini hata huko maisha hayakuwa na amani. Alinifanyia manyanyaso makubwa sana.

Hata baada ya kujifungua aliendelea kunifanyia ukatili na alitaka kuniingilia kingono hata nikiwa bado mzazi. Alipoulizwa kuhusu tabia hiyo alisema mimi nilikuwa malaya tangu zamani. Manyanyaso yalipozidi, niliamua kurudi kwa mama yangu. Lakini nilipofika, mume wa mama hakupenda tuwepo pale. Akaamua kutufukuza mimi, mama yangu na wadogo zangu. Usiku ule tuliomba hifadhi kwa jirani na tukalala huko.

Kuanzia hapo maisha yangu yalibadilika na kuwa ya mateso zaidi. Nilikuwa bado msichana mdogo tayari nina mtoto, na ilinibidi nitafute kazi ili nijikimu na kumlea mwanangu. Katika kipindi chote hicho, sikuweza kumshirikisha mtu mwingine zaidi ya mama yangu. Watu wengi niliotaka kuwaambia walikuwa wananilaumu mimi badala ya kuona kuwa nilikuwa mtoto mdogo niliyeshindwa kujitetea dhidi ya watu wazima waliokuwa wananitumia vibaya.

Katika yote hayo niliyopitia, namshukuru Mungu kwamba sijawahi kupata maambukizi ya UKIMWI. Mama yangu alinisimamia mara kadhaa nilipomhitaji huu ndio ulikuwa msaada wangu. Pia nilipata msaada kutoka kwa mashirika kama ANGAZA na WAJIKI ambayo yalinipatia mafunzo na kunisaidia katika baadhi ya mambo.

Leo nina watoto watatu, na mimi ndiye mwenye wajibu wa kuwahudumia kila siku. Ndiyo maana natamani kupata msaada wa kuanzisha biashara ili niweze kujitegemea na kuisaidia familia yangu.

Ujumbe wangu ni kwamba ukatili unaomkuta mtoto unaweza kubadili maisha yake yote.

MTOTO ANAPOKUWA MIKONONI MWA WATU WALIOPASWA KUMLINDA LAKINI BADALA YAKE WANAMTESA, MAKOVU YAKE HUBAKI KWA MUDA MREFU SANA.

Natamani kupata nafasi ya kuanza upya maisha yangu, nijitegemee na niweze kuwalea watoto wangu katika mazingira salama kuliko yale niliyopitia mimi.

HAKI KWA BINTI

- Catalina (Jina sio halisi)
- Nina miaka 19.
- Nilisoma mpaka darasa la saba..
- Nimetokea Dodoma. Ninafanya kazi za nyumbani.

Maisha yangu kwa sasa yanaonekana ya kawaida tu, lakini ndani yake kuna tukio ambalo lilibadilisha kabisa mwelekeo wa maisha yangu nikiwa bado mdogo sana. Mara tu baada ya kumaliza shule ya msingi, niliposhindwa kuendelea na masomo yangu, nilipata ujauzito, na kuanzia hapo maisha yangu yalichukua mwelekeo tofauti kabisa.

Kulikuwa na kijana mmoja ambaye nilimchukulia kama mpenzi wangu. Tulikuwa tunaishi katika kijiji kimoja, na kwa kipindi fulani tulikuwa tunaongea na kukutana mara kwa mara mtaani kama vijana wengine walio kwenye mahusiano.

Kijana huyo aliniahidi kwamba atanioa. Kwa sababu ya ahadi hiyo, nilimuamini sana. Kwa umri wangu wakati huo nilichukulia maneno yake kama ahadi ya kweli ya maisha ya baadaye. Niliona kama mtu ambaye angeweza kuwa sehemu ya maisha yangu na mtu ambaye ningeweza kujenga naye familia siku za usoni.

Siku moja alinipigia simu na kuniita niende nyumbani kwake. Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kufika katika nyumba anayoishi na kabla hatukuwahi kukutana katika mazingira ya faragha. Nilipofika mambo yalibadilika ghafla. Alinilazimisha kufanya mapenzi naye, ingawa sikutarajia jambo hilo. Alitumia nguvu na nilishindwa kumzuia.

Baada ya tukio hilo ndipo nilipopata ujauzito. Nilipogundua kuwa nina ujauzito nilihisi mshtuko mkubwa sana. Sikuwa nimejiandaa kuwa mama katika umri ule mdogo. Nilihisi hofu na kuchanganyikiwa, na sikuwa na uhakika wa nini kingetokea baadaye.

Nilipomweleza kuhusu ujauzito huo, alikataa kuhusika. Hakukubali kwamba mimba ile ni yake, na hakutaka kuwajibika kwa namna yoyote.Wazazi wangu walinishauri niachane naye na nianze kufikiria maisha yangu pamoja na mtoto niliyekuwa ninambeba. Kwa wakati huo nilijikuta katika hali ngumu sana. Nilikuwa bado mdogo na ninaitegemea familia yangu.

Hata hivyo, sikutoa taarifa ya tukio hilo mahali popote. Sikusema kuwa alinilazimisha kufanya mapenzi, hata kwa mama yangu mwenyewe. Nilichagua kunyamaza kwa sababu nilihisi aibu na sikujua ni wapi ningeweza kupata msaada au ni nani angeweza kunielewa.Katika jitihada za kutafuta msaada, nilijaribu hata kwenda kwa baba yake ili kuomba msaada. Baba yake alisema angezungumza naye, lakini alinieleza kuwa kijana huyo ana tabia ya kuwa mkali na si rahisi kumshawishi kuchukuwa majukumu ya kuwa baba wa mtoto.

Baadaye nilijifungua mtoto wangu, alikuja kunisaidia kwa kipindi kifupi tu hadi mtoto alipofikisha miezi miwili. Baada ya hapo hakuwahi tena kufika nyumbani kwetu wala kusaidia malezi ya mtoto. Nilibaki nikimlea mtoto wangu kwa msaada wa familia yangu. Wazazi wangu wamekuwa wakinisaidia kadri wanavyoweza. Mama yangu anamfahamu baba wa mtoto wangu, ingawa sikuwahi kumpatia maelezo ya kina kuhusu ukatili uliotokea siku ile. Baba yangu pia anamsimamia kama mjukuu wake.

Mpaka leo hii, mimi na baba wa mtoto hatuna mawasiliano yoyote, na hatuna mpango wa kuja kuoana siku za baadaye.

HAKUWAHI KUNITISHIA KUWA NISIMTAJE AU NISISEME CHOCHOTE. LAKINI KUTOKANA NA UMRI WANGU MDOGO WAKATI HUO, SIKUWA NAJUA NAMNA YA

Hadi sasa sijawahi kupata msaada wa ushauri nasaha.

Maisha ya kuwa mama katika umri mdogo si rahisi, lakini ninajaribu kufanya kadri ya uwezo wangu kuhakikisha mtoto wangu anakua katika mazingira salama. Wasichana wenzangu, ningependa kuwashauri wasidanganyike kirahisi. Si kila mtu anayesema anakupenda au atakuoa ana nia njema. Ni muhimu kuwa na malengo na kufikiria maisha ya baadaye kabla ya kufanya maamuzi makubwa.

MAOMBI YANGU KWA JAMII, TUNAOMBA WATU WATOE USHIRIKIANO KWA WAHANGA WA UKATILI WA KIJINSIA, HASA WASICHANA WADOGO AMBAO MARA NYINGI HUJIKUTA KATIKA MAZINGIRA MAGUMU BILA MSAADA. PIA NINAOMBA WATU WANAOFANYA VITENDO KAMA HIVI WACHUKULIWE HATUA

Mimi niko tayari kushirikiana na mamlaka husika ili haki ipatikane. Kikubwa ninachotamani ni kuona baba wa mtoto wangu anachukua majukumu yake ya kumhudumia mtoto wake. Pia ningependa kupata msaada wa kisaikolojia ili niendelee na maisha yangu vizuri.

MALIPO YA DENI LA BABA.

- Bimoza (Jina sio halisi)
- Nina miaka 17
- Nimesoma mpaka darasa la sita.
- Ninatokea Dodoma.

Nilikuwa naishi na mama yangu, mpaka siku moja baba yangu alikuja kunichukua. Alisema ananipeleka kwake ili niendelee na shule. Nilimwamini kwa sababu ni baba yangu. Nilidhani labda nitapata nafasi ya kuendelea na maisha ya kawaida ya mwanafunzi, hivyo nikaenda naye bila kusita.

Baba alikuwa anaishi katika kijiji kinachoitwa Mkondani. Nilipofika huko alinifikisha nyumbani kwake na nikakaa kama wiki moja. Baada ya hapo aliniambia twende kijiji kingine kinachoitwa Babayu. Tulipopanda gari kwenda huko, aliniambia ananihamisha shule.

Nilimwamini kwa sababu sikuwa na sababu ya kumtilia shaka. Lakini nilipofika ndipo nilianza kuelewa kuwa mambo hayakuwa kama alivyosema.

Badala ya kunipeleka shule, baba alinipeleka kwa mwanaume ambaye sikuwahi kumuona kabla maishani mwangu ili anioe. Nilishtuka sana.

Nilimwambia baba wazi kuwa sitaki kuolewa. Nilikuwa najiandaa kuingia darasa la saba na ndoto yangu ilikuwa kumaliza shule, lakini baba hakusikiliza. Badala yake alinambia kama nikirudi nyumbani hataki tena kunijua. Pia alinitishia kwamba anaweza kumfanyia mama yangu kitu kibaya. Maneno hayo yalinifanya ninyamaze.

Ilikuwa mwezi wa kumi na moja ndipo maisha yangu yalibadilika kabisa. Baba alinilazimisha kuolewa kwa mwanaume huyo. Nilihisi kama ndoto zangu zimechukuliwa bila mimi kupewa nafasi ya kuchagua.

Nilipofika kwa yule mwanaume alinipokea vizuri, kana kwamba tayari alikuwa ananifahamu. Wazazi wake hawakusema kitu chochote. Hapo ndipo nilipogundua kuwa baba yangu tayari alikuwa amewaeleza kila kitu.

Nilijaribu kumwambia baba yangu tena kuwa sitaki kuolewa, lakini hakunisikiliza. Aliniacha pale na kuondoka.

Sikukimbia kwa sababu sikuwa najua eneo lile na sikuwa na pesa wala nauli ya kurudi nyumbani. Nilikuwa nimeachwa pale bila msaada wowote.

SIKU YA KWANZA SIKULALA NA YULE MWANAUME. LAKINI SIKU YA PILI ALIKUJA PALE KWA WAZAZI WAKE NA KULALA NA

Nilikuwa naogopa sana na nilihisi kama sina mtu wa kunisaidia. Nilimwambia yule mwanaume umri wangu, lakini alisema yeye hataki kujua.

Baadaye ndipo niliposikia ukweli kwamba baba yangu alikuwa amechukua shilingi laki nane (TZS 800,000) kutoka kwake. Hapo ndipo nilipoelewa kuwa baba alinileta pale ili kulipa deni lake.

Baada ya muda nilipata nafasi ya kumpigia mama yangu simu kupitia jirani na kumwelezea ukweli wote. Mama yangu alienda kwa mwenyekiti wa kijiji ili kuripoti tukio hilo lakini kabla ya kuchukuliwa hatua yoyote, baba yangu alitoroka. Baada ya tukio hilo mama yangu aliamua kuachana naye kabisa.

Baadaye dada yangu alinisaidia kunitorosha kutoka pale. Niliondoka bila hata kuchukua vitu vyangu bali nguo nilizokuwa nimevaa tu. Nilipotoroka tayari nilikuwa mjamzito.

Sasa ninaishi kwa shangazi yangu ambaye si ndugu wa damu moja kwa moja na baba yangu, bali ni mke wa mjomba. Maisha huko pia si rahisi. Shangazi yangu mwenyewe ana maisha magumu na hakuna mtu anayenisaidia kipindi hiki cha ujauzito.

Dada yangu anajaribu kunisaidia kidogo kadri anavyoweza. Yeye anauza mboga. Nina kaka zangu wawili lakini hawakusema chochote kuhusu hali yangu.

Wakati mwingine nikikumbuka alichonifanyia baba yangu nahisi maumivu makali sana. Najisikia vibaya sana kwa sababu nimepoteza elimu yangu.

Nimebeba mimba nikiwa bado mdogo na sina mtu wa kunisaidia. Nilipoenda kliniki waliniambia lazima nije na mume wangu ili nipate kadi ya kliniki. Nilipowaambia sina mume walikataa kunipa kadi. Baadaye dada yangu alienda kuwaomba wahudumu wa afya ndipo walipokubali kunipa kadi ya kliniki.

KWA SASA UJAUZITO WANGU UNA MIEZI MITANO. NINA WASIWASI KUHUSU JINSI NITAKAVYOWEZA KUJIFUNGUA NA MUSTAKABALI WA MAISHA YANGU NA YA MTOTO WANGU.

Hata hivyo, bado ninajaribu kuwa na matumaini kuwa siku moja maisha yangu yatabadilika. Kwa watu wanaofanya mambo kama haya, naamini wanapaswa kuchukuliwa hatua kali za kisheria. Hata baba yangu mwenyewe ningependa achukuliwe hatua kwa sababu aliharibu maisha yangu.

KAMA NINGEPATA NAFASI, NINGEPENDA KUTOA TAARIFA ILI HAKI IPATIKANE.

Kwa sasa ninajaribu kuvumilia hali niliyopo na kuendelea mbele na maisha yangu.

NJIANI KURUDI NYUMBANI

- Careen(Sio jina halisi).
- Nina miaka 22.
- Nimesoma mpaka kidato cha nne.
- Ninatokea Dodoma.Ninafanya kazi ya upishi.

Kwa sasa ninaishi na bibi yangu mzaa mama kwa sababu wazazi wangu wote wawili walifariki dunia. Mimi sijaolewa, lakini nina mtoto mmoja. Ili kujipatia kipato cha kila siku huwa namsaidia mama mmoja kupika chakula sokoni siku za Ijumaa, na siku nyingine ninauza karanga za kukaanga ili kupata fedha za kujikimu.

Tukio lililonibadilishia maisha lilitokea mwaka jana mwezi wa tisa. Wakati huo nilikuwa nimeondoka Kigwe na kwenda Dodoma mjini kufanya kazi za ndani kwa mama mmoja mwenye umri mkubwa kama bibi.

Siku moja alinituma dukani kununua vitu kwa ajili ya wageni waliokuwa wamefika nyumbani. Dukani kulikuwa na foleni kidogo, hivyo niliporudi ilikuwa tayari usiku kama saa mbili hivi. Nilipokuwa narudi nyumbani nilipita kwenye kichochoro fulani ndipo nikakutana na wanaume wawili. Waliniuliza natoka wapi, nikawaambia natoka dukani. Kisha wakaniuliza nina pesa kiasi gani, na nilipowaambia sina kitu wakaanza kunipiga.

MMOJA WAO AKANIBAKA, NA NILIPOANZA KUPIGA KELELE YULE MWINGINE AKANIZIBA MDOMO KWA KITAMBAA NA KUNIFUNGA ILI NISIPIGE KELELE. BAADA YA YULE WA KWANZA KUMALIZA, YULE WA

Walipomaliza, walikimbia na kuniacha pale. Nilipiga kelele lakini majirani hawakutoka. Katika eneo lile watu wengi wanaogopa kutoka usiku kwa sababu wanaamini unaweza kutoka kusaidia halafu ukafuatwa wewe mwenyewe. Baada ya tukio lile nilikaa kimya kwa muda mrefu bila kumwambia mtu yeyote. Nilihofia kuulizwa ni nani waliofanya tukio hilo kwa sababu nilikuwa mgeni pale na sikuweza kuwatambua vizuri. Siku ile nilirudi nyumbani kwa kuchelewa na mwajiri wangu aliniona na kunikemea. Nilimwambia kulikuwa na foleni dukani. Baada ya kuwatengenezea wageni chakula niliingia chumbani kwangu na sikuweza hata kula chakula siku hiyo.

Baada ya muda nilianza kuumwa ndipo nikaamua kurudi nyumbani kwa bibi yangu Kigwe. Nilipofika hali yangu iliendelea kuwa mbaya, hapo ikabidi nipelekwe hospitali ambako vipimo vilionyesha kuwa nilikuwa na ujauzito pamoja na magonjwa ya zinaa. Nilitibiwa magonjwa ya zinaa na mimba ikaendelea. Baadaye nilijifungua mtoto wangu. Baada ya tukio hilo nilisikia kwamba katika kile kichochoro tukio kama hilo liliwahi kutokea hapo awali, na kuna mtu aliwahi hata kupoteza maisha baada ya kufanyiwa ukatili pale. Kwa sababu ya aibu na hofu nilikaa kimya kwa muda mrefu, hadi bibi aliponiuliza ndipo nilipomweleza kilichotokea.

TUKIO LILE LILINIACHA NA MAUMIVU MAKUBWA MOYONI. NILIPATA MSONGO MKUBWA WA MAWAZO NA MARA NYINGI NILIKUWA NIKIKAA PEKE YANGU CHUMBANI NA KULIA NIKIKUMBUKA KILICHOTOKEA.

Kazi yangu ya Dodoma pia ilibidi niache. Msaada niliopata ulikuwa kutoka kwa mjomba wangu ambaye alinisaidia kunipeleka hospitali na kupata matibabu, na baada ya hapo nilianza kuhudhuria kliniki kwa sababu huduma za wajawazito hutolewa bure. Hata hivyo maisha hayakuwa rahisi.

Katika jamii baadhi ya watu walikuwa wakisema maneno ya kunidharau wakisema mtoto mwenyewe hata baba yake hajulikani. Hata hivyo familia walielewa kwamba lilikuwa tukio la bahati mbaya na kwamba sikufanya kwa makusudi.

Sikutoa taarifa polisi kwa sababu nilihisi ningeulizwa kuwataja waliofanya tukio hilo wakati sikuweza kuwatambua vizuri; ninachokumbuka tu ni kwamba mmoja alikuwa na mwili mkubwa kidogo na mwingine alikuwa mwembamba mrefu.

Baada ya kujifungua pia nilipata matatizo ya kiafya. Nilishonwa hospitalini lakini nyuzi zilifumuka na ikabidi nirudi tena kushonwa upya. Hata hivyo bado kuna sehemu ambayo haijapona vizuri, na wakati mwingine maji hutoka bila kujizuia.

Niliambiwa niende hospitali ya rufaa kwa matibabu ya madaktari bingwa lakini sijafanikiwa kwenda kwa sababu ya gharama. Ni miezi minne sasa na bado siko vizuri.

KWA SASA MSAADA NINAOUHITAJI ZAIDI NI WA KIAFYA ILI NIPATE MATIBABU SAHIHI, NISHONWE VIZURI NA NIPONE KABISA. PIA NINAOMBA HUDUMA KWA MANUSURA WA UKATILI ZIBORESHWE, KWA SABABU WAKATI MWINGINE MTU ANAKUWA AMEJERUHIWA VIBAYA LAKINI MATIBABU HAYAFANYIKI

Ninawasihi waajiri waishi na wafanyakazi wao kwa upendo. Mwajiri akiwa mkali sana inakuwa vigumu kwa mfanyakazi kueleza changamoto anayopitia.

Wazazi wana umuhimu wa kufuatilia maendeleo ya watoto wao wanapokuwa wameajiriwa mbali na nyumbani. Pia Jamii naiomba iache kuwadharau wanawake wanaopitia changamoto kama hizi na badala yake watoe ushirikiano na msaada.

Ninashauri mamlaka husika kufuatilia kesi za ukatili wa kijinsia kwa haraka ili tabia hizi zikome. Ninawatia moyo manusura wengine wa ukatili wa kijinsia wa kingono kuvunja ukimya na kuzungumza ili waweze kupata msaada.

Pia, ninaomba kupata msaada wa kisaikolojia utakaoniwezesha kuendelea kupona na kuanza upya safari ya maisha yangu.

UKATILI UNAOFANYWA NA MWALIMU

- Isabella (Sio jina halisi)
- Nina miaka 18.
- Nilisoma mpaka kidato cha kwanza.
- Ninaishi Dodoma. Ninafanya kazi za nyumbani.

Nilikuwa naishi na mama yangu na nilikuwa na ndoto kubwa ya kusoma kama watoto wengine. Nilikuwa naendelea vizuri na masomo yangu mpaka maisha yangu yalipobadilika nikiwa bado mdogo sana. Nilipokuwa nasoma shule ya msingi darasa la nne, kulikuwa na mwalimu mkuu ambaye alikuwa na tabia ya kuwalazimisha wanafunzi wa kike kuwa naye kimapenzi.

Alikuwa akinitaka mara kwa mara, lakini nilikuwa nikimkataa kwa sababu sikuwa naelewa kabisa mambo hayo na nilikuwa natamani tu kuendelea na masomo yangu kama kawaida.

Nilipofika darasa la saba hali ikawa mbaya zaidi. Kipindi hicho tulikuwa tunaandaliwa kwa ajili ya mtihani wa taifa kupitia kile tulichokiita "kambi." Kambi hizi hazikuwa kama shule za bweni. Badala yake, wanafunzi tulibaki shuleni na kulala kwenye madarasa yale yale tuliyokuwa tunasomea. Hakukuwa na vitanda; tulilala kwenye mikeka. Baadhi ya madarasa yalikuwa na milango lakini mengine hayakuwa nayo kabisa. Tulikuwa tunachangisha wenyewe mahindi na maharage ili tupate chakula.

Hakukuwa na sehemu za kujisitiri kati ya wavulana na wasichana, na vyoo vilikuwa vile vile vinavyotumiwa na shule nzima, mara nyingi vikiwa vichafu. Maji pia hayakuwa ya uhakika; wakati mwingine tulilazimika kwenda kuchota maji mbali kwenye visima vya watu, na kama wenye visima hawapo tulikuwa tunaiba maji ili tuweze kuoga. Ndoo moja ya maji ilitumiwa na watu kadhaa kuoga. Hata wasichana waliokuwa kwenye siku zao walilazimika kutumia mazingira hayo hayo. Kwa ujumla, mazingira ya makambi yalikuwa magumu na yasiyo salama kabisa.

Katika mazingira hayo, mwalimu mkuu alianza kunilazimisha kuwa naye kimapenzi. Nilipomkataa alinipa uongozi shuleni na kunifanya "Dada Mkuu" (Head Girl), pamoja na kunipa funguo za shule. Lakini kila nilipokuwa nikipeleka funguo jioni, alikuwa ananitaka kufanya naye mapenzi. Alikuwa akinitishia kwamba nikikataa angenifukuza shule, au angewaambia wazazi wangu kuwa nimefanya kosa kubwa ili nifukuzwe. Nilitamani sana kusoma, hivyo niliogopa kusema chochote.

OFISINI KWAKE KULIKUWA NA SOFA AMBAPO MARA NYINGI ALIKUWA ANANIVUTA NA KUNIDONDOSHA HAPO NA KUFANYA ALICHOTAKA KWENYE MWILI WANGU.

Baada ya hapo nilirudi darasani lakini nilikuwa nashindwa hata kusoma kwa sababu ya hofu na msongo wa mawazo.

Hakunifanyia mimi peke yangu, bali wasichana wengi walipitia hali hiyo. Wakati mwingine alikuwa anawalazimisha hata watoto wadogo sana.

Tulijua sisi kwa sisi kinachoendelea, lakini hakuna aliyethubutu kusema chochote. Alikuwa ametutisha kwamba kama mtu yeyote angesema, angewafukuza shule wote. Mara nyingi alikuwa anawaita wasichana mmoja mmoja.

Nilipoitwa nilijaribu kwenda na rafiki yangu, lakini akituona wawili alikuwa anamtuma mwenzangu dukani au kutafuta maji. Duka lilikuwa mbali na shule na wakati huo shule nzima ilikuwa kimya. Walimu wengine walikuwa wanaishi mbali; ni mwalimu mkuu na mke wake tu waliokuwa karibu na shule. Hata hivyo mke wake hakuwa anafuatilia kinachoendelea, kwani alikuwa anakuja kufundisha darasa la kwanza kwa muda mfupi na kisha anarudi nyumbani.

Baada ya kumaliza darasa la saba nilifaulu na nikajiunga na kidato cha kwanza. Hata hivyo, nilipofika kidato cha kwanza ndipo niligundua kuwa nina ujauzito. Kufikia wakati huo mwalimu alikuwa amenifanyia vitendo hivyo mara nyingi sana. Nilikuwa na miaka 15 tu. Nilijaribu kuendelea kusoma kwa muda, lakini kadri ujauzito ulivyokuwa unaendelea kukua nilianza kujisikia vibaya na hata kutapika darasani. Mwishowe nililazimika kuacha shule na kurudi nyumbani.

Sikumwambia mtu yeyote kuhusu ujauzito huo. Mama yangu ndiye aliyegundua mabadiliko kwenye mwili wangu na kuniuliza nini kilikuwa kinaendelea. Nilimwambia kuwa hata mimi sielewi. Baadaye alinipeleka kwa nesi ambapo vipimo vilionyesha kuwa nilikuwa na ujauzito. Nyumbani kulizuka mgogoro mkubwa. Kaka zangu walitaka kunifukuza nyumbani, lakini baba yangu aliwakataza. Alisema, "Sasa ataenda wapi?" Wengine walitaka mimba itolewe ili nirudi shule, lakini baba yangu alikataa. Alisema mtoto aliyeko tumboni pia ana haki ya kuishi.

Baada ya hapo nilibaki nyumbani. Kaka zangu waliendelea kunilaumu kwa nini sikusema mapema. Nilijaribu kuwaelezea kuwa nilikuwa naogopa, kwa sababu mwalimu alikuwa ananitishia kuwa nikisema angefanya nifukuzwe shule. Nilikuwa natamani sana kusoma, na hofu hiyo ilinifanya ninyamaze kwa muda mrefu.

Baadaye kaka zangu walienda kutoa taarifa polisi na kuanza kumtafuta mwalimu huyo. Hata hivyo mpaka leo sijui walifikia wapi na suala hilo. Wakati huo pia sikupelekwa katika kituo cha afya kupata msaada wowote. Kilichoniumiza zaidi ni kwamba nilikuwa natamani sana kusoma, lakini ndoto hiyo ilikatishwa ghafla. Mwalimu huyo pia alinipotezea usichana wangu nikiwa bado mdogo sana. Hadi leo bado ninaumia ninapokumbuka kilichotokea.

UJUMBE WANGU KWA WASICHANA WENGINE NI KWAMBA WAKIKUTANA NA MAMBO KAMA HAYA WASINYAMAZE. NI MUHIMU KUTOA TAARIFA MAPEMA KWA WATU WANAOWEZA KUSAIDIA.

Mimi nilinyamaza kwa sababu ya hofu.

Pia ninaamini mfumo wa makambi ya wanafunzi unapaswa kufikiriwa upya, kwa sababu wakati mwingine unatoa nafasi kwa baadhi ya walimu kuwanyanyasa wanafunzi. Kama makambi yataendelea kuwepo, basi ni muhimu kuwe na ulinzi wa kutosha na uwepo wa walimu wa kike ambao wanaweza kuwasaidia na kuwalinda wasichana. Ninaamini kwamba kama watoto watalindwa na kusikilizwa mapema, wengi wao wataweza kuendelea na ndoto zao za elimu bila kuvunjwa na ukatili.

MATOKEO YA KUDUMU YA UTOTO ULIOPORWA

- Michelle (Sio jina halisi).
- Nina miaka 33.
- Nimesoma mpaka kidato cha nne.
- Ninaishi Dar es Salaam.

Mimi ni mtoto niliyezaliwa katika mazingira ambayo mama yangu na baba yangu ni watoto wa kambo. Babu na bibi yangu walioana kila mmoja akiwa na mtoto wake; hao watoto ndio mama na baba yangu. Baadae walianzisha mahusiano yaliyopelekea mimi kuzaliwa. Babu yangu hakupendezwa na kitendo hicho na hivyo alihakikisha wanaachana.

Baada ya mama na baba kuachana, maisha yalibadilika na kuwa magumu, kiasi ambacho mama alishindwa kunilea na kunipeleka kwa bibi yangu ili niweze kupata mahitaji muhimu. Kipindi hicho nilikuwa na umri wa mwaka mmoja na nusu.

NILIPOFIKISHA MIAKA MINNE, NIKIWA NAANZA KUPATA FAHAMU ZANGU, MBABU RAFIKI YAKE NA BABU YANGU ALIKUWA ANAKUJA NYUMBANI MARA KWA MARA. SIJUI ALIANZA LINI KUNIINGILIA KIMWILI ILA NILIVYOANZA KUJIELEWA NA KUPATA AKILI NILIKUTA ANANIFANYIA KITENDO HICHO.

Anapofika kama mgeni hupewa kigoda, anakaa na kunipakata katika mapaja yake huku akiwa ananiingilia kimwili. Japo watu wanakuwepo, hakuna aliyekuwa anaona anachonifanyia kwasababu inakuwa ni muda wa jioni na kijijini kuna giza. Alinilazimisha kukariri jina la maumbile yake ili nione ni kitu cha kawaida, niliamini kuwa watoto wote wanafanyiwa hivyo. Alikuwa ananiita "mchumba", na hata bibi na babu walikuwa wanamjua kama mchumba wangu.

Nina umri wa miaka 33 kwa sasa, lakini haya matukio ya ukatili dhidi ya watoto unapofanyiwa sio tu unalikumbuka, ila huwa linaharibu mfumo mzima wa maisha yako. Mfano mimi kuna wakati ninapita kwenye magumu, lakini najua tu sababu ni ule ukatili niliopitia; saa nyingine napitia changamoto kwenye mahusiano, lakini najua sababu ni yeye. Angeniacha nikautunza utu wangu au lahasha ningeutoa mwenyewe kwa hiyari yangu, labda ningesoma darasani kwa bidii, pia ningefanya mambo kutokana na utashi wangu, ila kutokana na hilo tukio, huo utashi wala sikuwa nao. Hali hiyo ilinipelekea mimi kukosa ujasiri, hata kufikia kushindwa kufanya maamuzi.

Katika umri wa miaka nane, maungo yangu ya uke hayakuwa tena kama ya mtoto. Mwanaume yeyote alikuwa anauwezo wa kuniingilia na kutoka bila shida. Tulipokuwa tunacheza ule mchezo wa kombolela, nilikuwa nakutana na wale watoto wenzangu, japo ilikuwa wakimaliza kufanya, naona hatujafanya kitu. Watoto wa kiume wote ambao waliwahi kuniingilia mimi kimwili walikutana na maumbile yangu ya kike hayafanani na umri wangu.

Nilipokuwa na miaka tisa nilikuwa natamani nipate mkaka mkubwa wakufanya nae ngono, kwasababu yule baba aliyenifanyia ukatili alikuwa amepotea kabisa na haji tena.

Changamoto ilikuwa kwa umri huo, sio rahisi kwa mkaka mkubwa kukutongoza, kwahiyo nilikuwa nakutana na vile vitoto vitoto.

Nilivyofika darasa la pili kama sio la tatu ilikuwa mwanaume awaye yeyote akinitongoza namkubali, sikuwa na ujasiri wa kusema hapana. Nilikuwa siwazi kuwa ninapata nini, na wala sikuwa na shida na hela, ni vile tu moyoni na akilini mwangu sikuwa naona thamani yangu tena.

Kuna kipindi wale walezi wangu wanaonilea walinikalisha chini wakaniambia kuwa *"Michelle usihangaike na wala usicheze na wanaume, ukicheza na wanaume tumbo litaumuka kama ngano"* wakiwa wanamaanisha nitapata ujauzito. Waliongea kwa kunijenga ila mimi nilikuwa nishaharibika ninaendelea tu na safari yangu ya ulimwengu na niliishi hivyo mpaka kufikia darasa la tano. Kipindi hicho nilikuwa ni msichana kabisa na naweza kulala na mwanaume yeyote yule.

Nilivyofika darasa la sita, nilipata mkaka ambaye alinitorosha nyumbani nikawa naishi naye kama mke na mume. Bibi yangu alienda kuripoti polisi ambapo alipewa majibu kuwa asiwe na wasiwasi, hakuna shida yoyote mjukuu wake atarudi. Nilipoteza kabisa matumaini ya kurudi tena shule au kufanya mtihani wa darasa la saba, maana hata zile fomu za maandalizi ya mtihani sikujaza. Ila mwalimu wangu alinijazia ili niweze kusajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba.

Maisha yangu kwa yule mkaka yalikuwa ya kufungiwa ndani, sikuruhusiwi kwenda kuoga au kuchota maji mwenyewe. Mwanaume mwingine akiniangalia nilikuwa napigwa kwanini mwanaume ameniangalia. Alinifundisha kunywa pombe na mimi nikawa mlevi sana. Tulikuwa tunaenda baa tukiwa tunakunywa ikitokea mimi nimeinuka na mwanaume mwingine ameinuka, napigwa kwamba tunawasiliana.

Siku moja mwalimu mkuu alimtafuta yule kaka na kumuomba aniruhusu kurudi kufanya mtihani maana zoezi la uandikishaji ameshalikamilisha. Alikubali na kuniletea vifaa vya kufanyia mitihani.

Siku ya mitihani alinisisitiza nijibu maswali ninayoyajua na nisiyoyajua niyaache. Nilipofika kwenye mtihani nikakuta maswali mengi nilikuwa nayajua na mimi nikajaza yote.

Matokeo yalivyotoka nilikuwa nimefaulu, na nilichaguliwa kwenda shule ya bweni ya wasichana tupu. Mama yangu aliamua kuja kijijini kunitafuta, alikutana na huyo mwanaume, na niliondoka na mama ila niliacha kila kitu changu kwa yule mwanaume.

Kwenye jamii yangu sikupata msaada kwa watu wengi zaidi ya bibi yangu na mama yangu kwa sababu jamii nzima pamoja na ndugu wengine walishanipa jina la mtoto mcharuko au nisiyekuwa na maadili kwa hiyo hakuna ambaye alikuwa anajali kuhusu mimi.

Huduma za msaada wa kitabibu kwa mara ya kwanza nilipata nikiwa tayari mtu mzima na akili zangu timamu. Nilivyopimwa sikukutwa na UKIMWI kwakweli nilifurahi sana.

Sitamani mtoto yeyote afanyiwe ukatili, unaweza kumfanyia mtoto ukatili na ukaona ni kawaida ila kwa yule mtoto unamuharibia kabisa mfumo wa maisha yake. Hata kama mtoto alikuwa na kipaji hawezi tena kutimiza kile kipaji chake, maana tayari anakuwa na makovu ya kihisia na kisaikolojia. Mamlaka za serikali ziweke utaratibu mzuri wa kufuatilia na kufanyia kazi taarifa zinazotolewa ili kuokoa watoto wanaofanyiwa ukatili.

MFANO MIMI BIBI YANGU ALIKWENDA KURIPOTI POLISI ILA HAWAKUFANYA KITU NA NILIKUWA PALE PALE KIJIJINI, LABDA WANGENIOKOA KUTOKA KWENYE ULE UNYANYASAJI NA LEO NISINGEKUWA NAONGEA HIVI.

Pia, familia tuwe makini sana na watu wa karibu, mimi nilishawahi kuingiliana kimwili na kaka yangu mtoto wa mama yangu mkubwa. Jamii inajua kuwa ni kaka yangu ila mimi na yeye tulikuwa tunaendelea na mahusiano ya kimapenzi.Nimeshamuambia binti yangu hata kama ni baba yako, ukiona swala lolote linalohusisha mwili wako piga kelele kabla hata hujavuliwa nguo. Naongea kuhusu hata baba yake, kwasababu nayaona kwenye TV na kuyasikia.

NATAMANI SANA TUJUE HAYA MATUKIO KABLA HAYAJATOKEA, NA WATU WATOE TAARIFA MAPEMA. UKATILI UPO NA UNATISHA SANA.

KUGONGWA NA GARI



- Amara (Sio jina halisi).
- Nina miaka 38.
- Sijawahi kwenda shule.
- Ninaishi Tanga. Ninaendesha bajaji za walemavu.

Mwaka 2000 nilitongozwa na kaka yangu mtoto wa mama mkubwa nikamkataa. Mama yake na mama yangu ni baba na mama mmoja. Mwaka 2007 alinitongoza tena, nikakataa. Mwaka 2017, alijaribu kunibaka nikiwa kwao. Mama yake aliniita akiwa anaenda kwenye harusi, kwa mama yake na kwake ni jirani, na nyumba ilikua haina mtu.

Alikuja nyumbani kwa mama yake, akaniambia dada nenda kwangu kachukue nazi uje upikie, nikaenda. Mimi najua naenda nyumba haina mtu kumbe yeye anakuja nyuma nyuma. Tukavutana lakini mimi nikamzidi nguvu, nikafungua mlango nikakimbilia kule kwa mama yake.

Kumbe naye alikua ameshanikamia, akatoka kule akanifata huku kwa mama yake, akijiamini hakuna mtu.

Nilingia ndani nikihema bila hata kufunga mlango sikutarajia kama angenifata. Ile kanifika kuanza kuminyana baba yake akaja. Baada ya kusikia sauti, akaniacha, nikatoka nikaenda kwa kaka yangu mtoto wa mjomba. Nilimuelezea akaniambia atalifanyia kazi, sikujua walimalizana vipi.

Mnamo mwaka 2018, mama yake aliniita kwenye sikukuu ya Iddi nikaenda. Iddi ya tatu alikuja na gari ndogo tukasalimiana. Wakati akiingia alinitishia kunigonga na lile gari ila eneo nililokua nimekaa nilikua pembeni ya mama yake.

MAMA YAKE ALIVYONYANYUKA KWENYE LILE ENEO AKAINGIA TENA KWENYE GARI, AKAJA AKANIBAMIZA NA GARI NA KUNISABABISHIA KUWA MLEMAVU MPAKA SASA HIVI.

Watu waliokuwepo katika lile tukio ilikua ni familia yake tu. Walivyonipeleka hospitali ya Makorola walisema ni ajali ya ukuta. Nilikua sijiwezi, sikuweza kuongea, kwahiyo hospitali walikubali walivyosema nimedondokewa na ukuta.

Nilivyotoka pale, nikaenda na ripoti ile mpaka hospitali ya Bombo, Tanga mjini wakanipokea. Nilikaa siku nne ndipo nikapewa rufaa kwenda hospitali ya Muhimbili. Walinipokea na walijua ni ajali ya ukuta lakini haikua ajali ya ukuta, ilikua ni ajali ya gari.

Mama yangu nilimueleza badae, ila mama mkubwa alikuwepo kwenye tukio. Wakati nipo chini ya uvungu wa gari mama mkubwa alikuwa ananiona na hakufanya kitu. Hospitali nilipelekwa na majirani na mlengwa mwenyewe. Alikuja kaka yangu mwingine mtoto wa mjomba lakini alikuta tayari nimeshawekwa pembeni, wametulia.

Niliporudi nikawa na mpango wa kufungua kesi kwasababu nilikua sijiwezi tukio lilivyotokea.

Sikuzimia ila nilikua siwezi kutoa sauti, nilikua nimeumia kwenye uti wa mgongo. Kuongea kwangu ilikua mpaka uje uweke sikio lako kwenye mdomo ndio unielewe, lakini matukio yote nilikua naona na kusikia kila kitu.

Pia, kuhema nilikua siwezi vizuri kwasababu alinigonga mbavu zote mbili, alinigonga kinyume nyume, akaniganyaga ubavu, alafu akaenda mbele akakanyaga tena ubavu wote.

Mpaka leo hii hanisalimii. Majirani waliona ila sijajua walilielezea vipi hili tukio, sababu sikuwepo. Tukio lilitokea mwezi wa sita na nilitoka hospitali mwezi wa nane mwishoni.

Tukio hili limeniathiri kutokana na mazingira magumu ninayo pitia kifedha. Siwezi tena kufanya biashara yangu ya kutembeza dagaa maana siwezi kutembeza. Mama yangu ni masikini, natakiwa kurudi tena Muhimbili kliniki ili waangalie kama kifaa walichoniwekea kiko sawa, au hakiko sawa.

Hakuna kikao chochote cha familia kilichokaliwa kuhusiana na tukio hili na hakuna msaada niliopata kutoka kwa ndugu. Polisi nilishawahi kwenda lakini polisi niliyemkuta aliniambia muda umekwenda, na kwamba inatakiwa kutoa taarifa ndani ya siku saba. Pia, changamoto ni huo ushahidi hakuna. Maana hakuna wakusimama wa kutoa ushahidi kwa ndugu yake.

BAADA YA AJALI, MUME WANGU ALINIACHA. HAKUTAKA KURIPOTI POPOTE, YEYE ALIVYOONA IMESHAKUA HIVI AKAAMUA TUACHANE. HAJAWAHI KUFIKA HOSPITALI HATA MARA MOJA.

Ninapitia hali ngumu bila msaada wa familia. Bila msaada, siwezi kuhimili gharama za hospital au mazoezi hivyo naishi kwa kuvaa pampasi. Mtu ananiona nimependeza lakini napitia changamoto, mtu wa nje hawezi kujua, labda watu walio karibu na mimi.

Sababu yeye hataki kunipa msaada ningependa tu, sheria ifate mkondo wake. Yaani ni mtu aliye niharibia maisha yangu. Na yeye yupo njiani anaendelea na maisha yake kama vile hakuna kilichotokea, ikiwa mwenzake naumia, mimi ndie ninaye teseka.

JAMII NA FAMILIA ZIJIFUNZE KUTOKA KWENYE HILI LILILONITOKEA MIMI. MAMBO KAMA HAYA ISITOKEE YAKAMALIZIKA KIFAMILIA MAANA MATOKEO YAKE NI MADHARA MAKUBWA.

Kama hili walisema limalizike kifamilia, matokeo yake inanigharimu mimi. Mama yangu hakushirikishwa kwenye maamuzi hivyo hasemi lolote.

Natakiwa kufanya mazoezi ya kunyooshwa pale hospitali ya Bombo. Kuna kitanda cha kusimamia, na kila ninapoenda ninatakiwa nilipe 15,000 na mimi sina bima.

UBAKAJI UNAPOSABABISHA NDOA YA UTOTONI

- Najma (Sio jina halisi).
- Nina miaka 27.
- Nilisoma mpaka darasa la saba.
- Ninaishi Tanga. Muuzaji wa vyakula

Nilivyomaliza shule nilikuja Tanga, huku nilipata mwanaume akanizalisha mtoto mmoja kwanza kabla ya kunioa. Baada ya kupata mtoto alikuja nyumbani akasema "nataka nimuoe awe mke wangu." Familia yangu ilikubali, ndio akanioa kabisa. Nilipokuwa naishi naye ndio nikapata mtoto wa pili.

Kipindi ananitaka alimwambia dada kuwa anataka kutoka na mimi, ndio tukaondoka. Mimi wakati naenda sikujua anaenda kufanya nini. Aliniambia naenda kumuona mama yake, lakini hakunipeleka kwao bali nyumbani kwa rafiki yake. Kila mara nilipomuuliza alinijibu "mama anakuja sasa hivi" mpaka jua linazama.

Usiku nikamwambia anirudishe nyumbani akaniambia hapana, nitakurudisha bado, kumbe yeye alikua na nia ya kuniingilia.

Hili ni jambo la ukatili maana mimi mwenyewe sikutoa ridhaa, alinilazimisha kile kitendo. Huyu mwanaume kwa kipindi hichi ni kama alinibirisi, maana ilikua bado hata sijaingiliwa. Nilirudi nyumbani nikasema kwa dada, ambaye alimpigia mama yangu. Yule mwanaume alipoitwa akasema "ni kweli nimefanya hicho kitendo lakini sitomuacha nitamuoa", ndio akanioa. Wakati huo nilikua na miaka 15. Hili tendo lilinikera ila sikwenda kushitaki polisi mimi nilienda kushitaki kwa wazazi.

TULIENDA HOSPITALI NA WAKATHIBITISHA NIMEINGILIWA NA WAKANIPA DAWA YA MAUMIVU. PALE NYUMBANI PIA KUNA WATU WAZIMA, WAKANIAMBIA NIWE NANAWA NA MAJI YA MOTO, NA NISIENDE TENA MPAKA ATAKAPO KUJA KUNIOA.

Baada ya hapo aliendelea kuja na kunihudumia. Tulimaliza kifamilia kwa ahadi ya kunioa.

Aliendelea kuja nyumbani lakini hatukuwa tunafanya mara kwa mara. Baada ya muda nilipata mimba alihalalisha akanipeleka kwake na kwamba nikiwa na shida niende hapo, aliniaminisha kila kitu. Alisubiri nijifungue ndio akaja kusema mimi namuoa sasa.

Baada ya kuingia katika maisha ya ndoa alibadilika na kuanza kunipiga na kurudi usiku, nikienda kusema nyumbani anakanywa. Alivyo nipiga mara ya mwisho ndio nikasema hapa basi, jicho lilikuwa jekundu, nikaamua kwenda polisi. Walimuonya wakamwambia ukimpiga tena utalala ndani. Akasema "mimi simpigi tena", wakamwambia ukimpiga tena, talaka utaandika hapa hapa na kumpa.

Pamoja na lile onyo, alirudia tena kwa kunipiga na mkanda, mimi nikaenda tena polisi. Niliwaambia polisi nimechoka na kuwaomba wamwambie aniandikie talaka yangu mbele yao anipe. Akaambiwa sasa hapa andika tu talaka. Akaniandikia talaka moja nikarudi nyumbani.

ATHARI ZA KUOLEWA KATIKA UMRI MDOGO NI KUBWA, NIMEPITIA UKATILI WA KIMWILI KAMA KUPIGWA, MPAKA KUNA KIPINDI NILIKUWA NIKIKOHOA NATEMA DAMU, NIKAENDA HOSPITALI NIKAPEWA DAWA. MUME WANGU ALINILAZIMISHA KUKAA NDANI, AKINIKUTA NJE TU NI MAKOFI.

Ijapokuwa mimi kukaa nje ilikuwa na wenzangu pale pale nyumbani.

Ninakosa huduma za watoto. Kama mtoto kaumwa naangaika mwenyewe na ndio maana na mimi nikatafuta kibarua, nipate angalau mia mbili, kusaidia kukaa na watoto. Baada ya mume wangu kutoroka, sasa hivi naishi na watoto tu, na nyumba kaiacha wanakaa familia yake nyingine.

Wapo walionilaumu kwamba nimeanza angali bado mdogo, maana nimezaa huyu mwanangu sina maziwa. Wakawa wananilaumu kwanini nimekubali kuzaa mapema, niliwajibu "imeshatokea na nisingeweza kutoa mimba ningali bado mdogo". Sikuwa nampenda lakini alishaniharibia maisha yangu, hivyo alivyoniambia atanioa basi nikatoa ridhaa.

Tangu nimeachana na mume wangu ni miaka mitano, na hata mahusiano yenyewe sina. Mwanzoni nilikua na hasira kwamba nimezalishwa, huduma sipati, watoto naangaika nao wenyewe ila kwa sasa hivi ninazingatia elimu na ustawi wao. Napata msaada kutoka kwa dada yangu ambaye ni mwalimu. Kipindi cha nyuma wazazi wake walinisaidia ila mama yake alifariki dunia.

Watoto wangu ni wakike hivyo nawaombea kwa Mungu kisiwakute kama kilicho nikuta mimi mama yao. Usalama wa watoto wangu nawalinda tu mwenyewe. Mmoja sasa hivi yupo darasa la tano, nawaambia wawe makini hasa miongoni mwa watoto wa kiume wanaowapa hela na vishawishi vingine, nikisisitiza umuhimu wa kufanya machaguo sahihi.

NATAKA WASICHANA WENGINE KUWA MAKINI NA WATU WANAOWAAMINI, KUTAMBUA JAMBO LINAPOONEKANAA SIO SAHIHI, KULIONGEA NA KUTAFUTA MSAADA. USALAMA WAKO NA SAUTI YAKO INA UMUHIMU.

Ukatili upo kweli, maana hata watoto wa kiume wameharibiwa, wanaingiliwa na wanaume wenzao wanaharibikiwa kabisa hiyo michezo ipo. Kuna siku nilimkuta kule mtaani mtoto wa kiume kwa mtoto wa kiume anamwambia mwenzake vua basi hiyo suruali, mimi nasikiliza, sasa avue suruali umfanye nini? Wakashtuka wakakimbia mimi nikaenda kwa mama yao maana namjua, nikamwambia mkanye mtoto wako, kama utanisikia sawa, na kama hauta nisikia sawa, kwa hiyo tabia hizo zipo.

MAPAMBANO DHIDI YA NDOA YA MATESO



- Kyra (Sio jina halisi)
- Nina miaka 50.
- Nilisoma mpaka darasa la saba.
- Ninaishi Tanga. Mjasiriamali.

Mwanzoni mwa ndoa yetu, nilikua naishi na mume wangu kwa amani. Baada ya miaka kadhaa, tabia yake ilianza kubadilika. Alianza kuja na mafuta ya nazi akitaka tufanye ngono ya kinyume na maumbile, ndio chanzo cha kugombana naye. Aliniingilia kinguvu kama mara 2 hata baada ya kukataa.

Hili lilinifanya kutafuta msaada kwa uongozi wa kanisa, kwa pamoja tuliitwa kukutana na mchungaji na mama mchungaji. Nilielezea changamoto niliyokuwa napitia ila baada ya kujieleza, mama mchungaji alisema nimemzalilisha yule mwanaume na hayo ni mambo ya siri na mapenzi ya kawaida. Iliniuma kwasababu ni kitu ambacho sijawahi hata kukifikiria.

Kipindi hicho hicho mume wangu alikuwa na mahusiano na wanawake wengine kama wanne hivi, akaniambia chagua wa kukaa naye mke mwenza, nilikataa. Akaniletea mke wa shemeji yake, alikua amefanyiwa upasuaji, tukae naye nyumbani kwetu.

Wakati huu kuna tukio lilitokea kuhusiana na matumizi ya familia. Nyumba yetu ilikua inatumia umeme wa kulipia ile mita ilivyokuja ilikua inadaiwa TZS 75,000/-. Kwa sababu pale ndani tulikua na mgonjwa aliyefanyiwa upasuaji nikaona nichukue TZS 30,000/- kutoka kwenye hela za mume wangu nikalipe ili nisikatiwe umeme. Alipogundua alikuwa mkali kupitiliza. Akachukua kanga akaninyonga kwenye shingo na anafunga kwenye tendego la kitanda, huku akiniambia utalipa hela yangu. Nikawa namuomba asiniue na kuahidii nitamlipa hela yake. Nilikua ninadeki yangu nimenunua TZS 60,000/- nikaiuza TZS 30,000/- nikampatia.

Ukatili uliendelea. Kwenye tukio lingine, usiku kwenye saa tatu, akaniambia usiniulize naenda wapi, naenda kwa mtu ambaye anaweza kunihudumia.

Alirudi kwenye saa sita za usiku, akaniambia kesho ninasafiri kwenda Moshi. Nikamuandalia vitu, baadae nikagundua anahama kidogo kidogoo bila mimi kujua. Nahisi yule mwanamke aliyekua naye ndio alimshawishi. Kufikia hapo nilikuwa nimekaa naye zaidi ya miaka 10.

Ukatili ulivyozidi na hali ya kupigwa mara nyingi, nilitafuta msaada kutoka shirika la kijamii linaloitwa Tree of Hope na nikatoa taarifa polisi. Alishikwa na kuwekwa kizuizini. Familia zetu ziliingilia kati, alikuja mjomba wangu nikakabidhiwa kwake na yeye akakabidhiwa kwa baba yake. Wakaambiwa kila mtu asikanyage kwa mwenzie.

Hata baada ya hayo ukatili uliendelea. Alishawahi kunipiga mpaka nikapelekwa kanisani, padre akasema hiyo kesi ni ya polisi. Hii Januari 2025 alinishambulia tena.

Alikuja akanilaza chini akasema ameenda kwa mganga mimi ndio nimefanya akienda kwa yule mwanamke hapati nguvu za kiume. Niliripoti tukio hili na aliwekwa kizuizini tena.

Hata hivyo marehemu baba yake aliomba tusuluishe nyumbani. Polisi waliendelea kumshikilia, baba yake alikutana na ndugu zangu, baada ya hapo akaachiliwa. Shambulio jingine lilitokea lililonifanya, niende hospitali ya Bombo. Baadae niligundua kuwa mume wangu alijaribu kuwashawishi madaktari waandike kuwa sina majeraha yoyote. Bahati nzuri wanajamii walinisindikiza hospitali ili kuhakikisha niko salama.

Ila baada ya kuniingilia kinyume na maumbile sikwenda hospitali na wala sikupata matibabu yoyote kwasababu nilikua natishiwa. Nilikua napata maumivu tu, baadaye hatua niliyochukua nikwenda kupima afya tu.

Ukatili niliopitia umekuwa na madhara makubwa kwenye afya yangu. Kuna siku alinishambulia vibaya sana, aliniumiza na nilikaa miezi saba hospitali ya Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC). Ili kuweza kulipa gharama za matibabu, nilijiunga na huu mkopo wa kinamama.

Sijawahi kupata ushauri nasaha kwa mtaalamu. Baada ya shambulio kubwa la tatu, niliamua kutafuta msaada wa kisheria ili nipate talaka yangu. Nikapewa barua niende kwenye kata, ambapo walisema inatakiwa nitoe hela na niwasilishe na cheti cha ndoa. Cheti cha ndoa kukifuatilia nikaambiwa kiko Korogwe. Nikafunga safari hadi Korogwe, ambapo niliambiwa kikao kilikaa mapema wiki hiyo, nikawa sina tena nauli ya kurudi. Kupitia makongamano ninayohudhuria, nimetambua kuwa wanawake wengi zaidi wanapitia mambo kama haya kwenye ndoa zao.

HILI AMBALO LIMENIKUTA JUZI, TULIPOFIKA NGAZI YA MAHAKAMA, NIKAAMBIWA NIPELEKE USHAHIDI NIKAKOSA USHAHIDI MAANA WALIKUA NI NDUGU ZAKE WALIOKUWEPO KATIKA LILE ENEO. ALIKUTWA HANA HATIA NA WAKANIAMBIA KAMA NAONA SIJATENDEWA HAKI NIKAKATE RUFAA.

UJUMBE WANGU KWA POLISI WANAPOKUJA MANUSURA WA UKATILI WA KIJINSIA WAWATENDEE HAKI. UCHUNGUZI UFANYIKE KWELI BILA KUPOKEA RUSHWA.

Manusura wapewe msaada wa kisheria hasa kwasababu ukatili wa kijinsia unafanyika ndani sasa na hivyo ushahidi ni ngumu kupatikana.

WITO WANGU KWA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NI KUTENDA KWA UADILIFU. WATOA HUDUMA ZA AFYA WASIPOKEE HONGO ILI KUBADILISHA RIPOTI. HAMNA MTU ANAENDA KUMSHITAKI MTU MWINGINE BILA SABABU.

Nimeishi na huyu mwanaume kwa miaka ishirini kama ningekuwa mbaya ile miaka miwili tu ingetosha. Nimeondoka hajanipa chochote na bado mateso yanaendelea, haipendezi.

Ujumbe wangu kwao wanaopitia ukatili wa kuingiliwa kinyume na maumbile katika ndoa ni wasikae kimya. Wasikae ndani na kusuluhishwa tu kama mimi, mwishoni yanarudi pia kwa watoto na vizazi vyetu. Ninachoomba watoke waende wakajieleze kwenye vyombo vya sheria.

PIA WATU WASING'ANG'ANIE NDOA AMBAZO SIO SALAMA AU HAWATHAMINIKI. NI BORA KUTAFUTA NAMNA YA KUISHI KWA UWEZO WAKO MDOGO KWENYE USALAMA KULIKO KUENDELEE KUNG'ANG'ANIA MWENZA MBAYA.

Jamii naiambia kwa kweli waache ukatili. Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kulindwa. Tunapoona vitendo vya ukatili katika jamii, tukaripoti, na watu wanaofanya ukatili wachukuliwe hatua.

MAISHA NA MAAMBUKIZI YA VVU

- Mina (Sio jina halisi).
- Nina miaka 23.
- Nimesoma hadi kidato cha pili.
- Ninaishi Dar es Salaam. Mimi ni mama lishe.

Nilizaliwa katika Mkoa wa Mwanza. Kwetu tulizaliwa watoto tisa, na mama yetu hakuwa na uwezo wa kutusomesha. Ndio akanipeleka nikaishi kwa mama mkubwa wangu, ili niendelee na masomo. Wakati ananipeleka akaniambia hawa watu wameathirika na huu ugonjwa wa sasahivi akanisisitiza nikae kwa umakini. Niliogopa sana, nilitaka kubaki ila kutokana na maisha ya nyumbani sikuwa na jinsi, ilibidi nikubali kuishi pale na nikaendelea na masomo yangu. Wakati huo nilikuwa bado nasoma shule ya msingi na nilikuwa na ndoto ya kuendelea na elimu yangu.

Siku moja mama mkubwa alikuwa amekwenda kanisani kwenye mambo ya kwaya. Nyumbani nilibaki na yule baba mkubwa, alianza kuniambia kuwa anataka kufanya mapenzi na mimi ila nilikataa.

Alichukua hatua ya kunifunga kamba mguu mmoja upo kule mwingine upo kule, kama mnyama na kuniingilia kwa nguvu na kunibaka.

Baada ya kumaliza akaniambia nikijaribu kumuambia mtu ataniuwa. Niliogopa na sikumuambia hata mama, ila mama aliniona nimebadilika sipo kama kawaida. Alikuwa ananiuliza kwanini nipo tofauti, mbona naonekana kama nimeanza kujiingiza kwenye mahusiano, nikamuambia hakuna kitu. Hapo nilikuwa darasa la nne, niliishi kwa unyonge sana, na sikuwa na uwezo wa kumuambia mtu, kilichonitokea.

Siku zilipita nikaanza kuugua mkanda wa jeshi, ulianzia huku mgongoni. Mama alivyoona ikabidi anipeleke hospitali,

NILIVYOFANYIWA VIPIMO NIKAKUTWA NINA MAAMBUKIZI YA VVU. ALIPONIULIZA NIMEUPATA WAPI IKABIDI NIMUELEZEE BABA MKUBWA ALIVYONIBAKA.

Mama aliumia sana, alilia sana ila hakuwa na chakufanya maana ilikuwa imeshatokea.Ikabidi niondoke na kwenda kwa dada katoro ili kupata lishe nzuri. Muda ulivyozidi kwenda akaanza kuninyanyasa, nakunisema kuwa nimeanza umalaya nikiwa mdogo ndio maana nimepata VVU, japo alijua fika chanzo cha ugonjwa wangu. Yale maneno yalikuwa yananiumiza sana na yalivyozidi ikabidi nitoroke na kwenda kahama machimboni kwenye madini kufanya kazi.

Niliondoka na dawa zangu za miezi sita, ilipofika baada ya mwezi mmoja niliibiwa begi langu likiwa na pesa na dawa zangu. Ilibidi nimuambie yule mama ambaye tulikuwa tunaishi kwake, na akanipeleka hospitali. Daktari alinipa dawa za mwezi mmoja na akanishauri nirudi nyumbani maana kadi yangu ilikuwa kwa dada.

Niliporudi nyumbani, dada yangu alikiri kuwa alikosea na aliomba msamaha kwa jinsi alivyonitendea. Niliishi naye kwa muda kabla ya kuamua kuja Dar es Salaam kutafuta fursa bora zaidi za maisha. Kuna dada mmoja alinitia moyo kuwa kutokana nakipaji changu cha kuimba na kuigiza, nikija dar nitafanikiwa kwa haraka. Nilipofika stendi ya basi ya magufuli, yule mwenzangu niliyekuja naye alinitelekeza pale stendi.

Wakati huo nilikuwa bado nakunywa dawa ila sikuwa na chakula wala sehemu ya kuishi. Kuna mama mmoja akaniona akanichukua kwake. Mazingira ya nyumbani kwake hayakuwa mazuri, maana alikuwa mume wake akija hata kama ni usiku mimi inabidi nikalale nje ili kuwapisha.

Baada ya muda nilipata kazi katika kibanda cha chips. Ikawa wakiondoka mimi ndio nalala pale pale. Usiku moja wakati nimelala wakatokea vijana watatu, wakaniwekea nguo mdomoni nisipige kelele na kunibaka , niliamka na maumivu ila sikuweza kumuambia mtu.

Baada ya wiki kadhaa kupita niliona hali yangu ya kiafya inabadilika, nikaenda hospitali wakanipima na kukuta nina ujauzito. Nilihisi dunia nimeibeba mabegani kwangu, nililia sana ile siku, nikifikiria wale wakaka walionibaka siwajui, na wala kati yao ni nani alikuwa mhusika. Nikaangalia sina mahali pakulala.

Licha ya hali hiyo, nikaendelea na kazi yangu na kulala pale pale kwenye kibanda cha chips, mazingira hayakuwa mazuri kwa kutunza mimba. Siku moja nilianza kutokwa na damu ghafla na kupata maumivu makali tumboni. Mwanaume mmoja aliyekuwa anaishi karibu aliona hali yangu na kuniuliza kilichokuwa kinatokea. Alinisaidia kunipeleka hospitalini na akalipia matibabu yangu. Baadaye pia alinisaidia kupata chumba kidogo cha kupanga Manzese. Kutokana na msaada wake alioutoa katika wakati mgumu wa maisha yangu, sasa namchukulia kama kaka yangu.

Baada ya kupona, niliweza kupata kazi maeneo ya Shekilango ambayo inanisaidia kulipia kodi ya chumba na mahitaji yangu ya msingi. Sambamba na kazi hiyo, bado ninaendelea kujaribu kuendeleza vipaji vyangu vya kuimba na kuigiza nikiwa na matumaini kuwa siku moja vitanifungulia fursa bora zaidi za maisha.

Sijawahi kupata msaada wowote wa kisaikolojia. Kutokana na kutokuwa na imani na watu. Kuna wakati nilimweleza rafiki yangu kuhusu hali yangu, lakini alisambaza siri yangu kwa majirani kwa kuwaonyesha dawa zangu. Tukio hilo liliniumiza sana na kunifanya nipoteze imani kwa watu.

Hadi leo bado ninajiuliza kwa nini mjomba wangu alinifanyia ukatili ule. Mama mkubwa wangu mara-nyingi alikuwa mkali na wakati mwingine alinifanyia vitendo vilivyo umiza.

Kwa mfano, alipokuwa akimkata mtoto wake kucha, alinikatakata pia na wakati mwingine alinijeruhi bila kukusudia. Sijawahi kuelewa kikamilifu kwa nini alinitendea hivyo. Mbali na kumweleza mama yangu, sikuwahi kuripoti tukio la unyanyasaji kwa mamlaka yoyote kwa sababu nilihisi hakuna ambaye angeniamini au kunisaidia.

Hadi sasa hivi bado nina kovu lile la mkanda wa jeshi. Kila nikiliona najikuta nalia maana nakumbuka kile kilichotokea kule kwa baba mkubwa. Ninaogopa kuingia katika mahusiano ya kimapenzi. Wanaume wanapoona kovu hilo na kuniuliza lilitokana na nini, kumbukumbu za zamani hurudi tena.

Kama Kuna mkaka nilikuwa naye kwenye mahusiano, baadae akaja kugundua hali yangu ya kiafya. Badala ya kunielewa, alinifanyia ukatili na kunitishia kuwa angenidhuru ikiwa angeniona tena. Tukio hilo lilinifanya nijisikie kukataliwa na kukosa matumaini.

Wakati mwingine ninatafakari jinsi maisha yangu yangekuwa tofauti kama baba yangu angekuwa hai. Alikuwa na mali, ila alivyofariki ndugu zake wakazichukua. Mama akaanza kuishi maisha magumu. Msaada mkubwa niliowahi kupata ni matibabu na dawa za hospitali kwa ajili ya afya yangu. Zaidi ya hapo, mara nyingi nimekuwa nikitegemea nguvu zangu mwenyewe pamoja na msaada wa mara chache kutoka kwa watu wenye huruma.

UJUMBE WANGU KWA JAMII: WAZAZI NA WALEZI WANAPASWA KUWA WAANGALIFU SANA WANAPOWAKABIDHI WATOTO WAO KWA WATU WENGINE. USALAMA WA MTOTO HAUPASWI KAMWE KUWEKWA REHANI KWA SABABU YA UGUMU WA MAISHA. PIA KUNA HAJA KUBWA KWA JAMII KUCHUKUA JUKUMU LA KULINDA WATOTO NA KUWASAIDIA MANUSURA WA UKATILI KWA HESHIMA, HUDUMA SAHIHI NA MSAADA WA KISAIKOLOJIA ILI WAWEZE KUPONA NA KUENDELEA NA MAISHA YAO.

HADITHI HIZI ZINATUFUNDISHA NINI

Zikiangaliwa kwa pamoja, hadithi hizi zinaonyesha mifumo ambayo haiwezi kupuuzwa.

Zinaonyesha kuwa mara nyingi ukatili si tukio la ghafla tu. Mara nyingi hutokea taratibu kupitia ukimya, kuruhusu mambo yaendelee, uzembe, na mamlaka yasiyodhibitiwa. Katika matukio mengi, madhara hayakusababishwa na mtu mmoja tu, bali yaliendelezwa na mazingira yaliyowazunguka manusura kama vile nyumbani, shuleni, sehemu za kazi, jamii, na mifumo iliyoshindwa kuingilia kati.

Ukimya unaonekana tena na tena.
Ukimya unaotokana na hofu.
Ukimya unaotokana na aibu.
Ukimya una imarishwa na kutokuaminiwa, vitisho, au ahadi kwamba kusema ukweli kutafanya mambo kuwa mabaya zaidi. Katika hadithi nyingi, ukimya haukuchaguliwa kwa hiari; uliwekwa kwa lazima.

Mamlaka ni mada inayojirudia.
Mamlaka yanayohusiana na umri, nafasi ya uongozi, fedha, jinsia, elimu, au hadhi ya kijamii.
Mamlaka iliruhusu baadhi ya sauti zisikike zaidi na nyingine kupuuzwa au kutiliwa shaka.
Mamlaka ilisababisha kupinga kuwa hatari na kuripoti kuwa jambo la kuogopesha. Katika matukio mengi, tofauti ya mamlaka yenyewe ilikuwa silaha.

Mifumo ipo - hata pale ambapo haifanyi kazi.
Vituo vya polisi ambavyo havikuweza kuchukua hatua.
Vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoandika taarifa bila kutoa ulinzi.
Shule zilizohamisha tatizo badala ya kulitatua.
Familia na taasisi zilizochagua kulinda sifa badala ya usalama.

Madhara hayakuisha kwa sababu miundo iliyopaswa kushughulikia tatizo mara zote haikuwa tayari, haikufikika, au haikutaka kuchukua hatua.

Hadithi hizi pia zinatukumbusha kuwa kupona au kuendelea kuishi baada ya ukatili hakufuati njia moja. Hakuna njia moja sahihi ya kukabiliana na ukatili. Nguvu si lazima ionekane. Kupona si mchakato ulionyooka. Baadhi ya manusura walizungumza mapema. Wengine walibeba matukio waliyoyapitia kwa miaka mingi. Maamuzi haya hayapunguzi ukweli wa walichopitia/kustahimili.

Kinachoonekana wazi zaidi si udhaifu, bali ustahimilivu
Hadithi hizi haziombi huruma.
Zinaomba uwajibikaji.

Uwajibikaji wa kusikiliza.
Uwajibikaji wa kulinda.
Uwajibikaji wa kuhoji mila na mifumo inayoruhusu madhara kuendelea bila kuonekana.
Ikiwa kuna ujumbe mmoja unaobaki, ni huu:

Ukatili hustawi pale ambapo ukimya unatarajiwa.
Mabadiliko huanza pale ambapo kusikiliza kunageuka kuwa hatua.

WITO WA KUCHUKUA HATUA

Hadithi hizi haziishii hapa.
Zinaendelea katika kile tunachochagua kufanya baada ya kuzisoma.
Kusikiliza ni muhimu - lakini haitoshi.

JAMII NA WATU BINAFSI

- Zungumza pale unapotilia shaka kuwa kuna madhara, si hadi pale yanapothibitishwa.
- Pinga mila na imani zinazohalalisha ukatili au kunyamazisha manusura.
- Tengeneza mazingira salama yanayomwezesha manusura kuongea na kuripoti ukatili bila hofu.
- Acha kuwalaumu manusura kwa yaliyowatokea.
- Acha kuita ukatili “jambo la kifamilia”.

TAASISI

- Weka heshima, usalama na faragha ya manusura mbele.
- Chukulia kila taarifa ya ukatili kwa uzito na chukua hatua bila kuchelewa.
- Mifumo ya sheria na mahakama izingatie kutenda kwa mrengo wa manusura.
  Hakikisha huduma za matibabu zinapatikana bila malipo na kwa wakati.
  Imarisha huduma za msaada wa kisaikolojia na ustawi wa jamii.
  Ongeza wigo wa huduma za uhamasishaji na msaada wa kisheria bure katika wilaya zote.
  Ongeza na kufadhili nyumba salama kwa manusura.
  Hakikisha haki na msaada vinapatikana kwa wote na wahusika wanawajibishwa.

WAJIBU WETU

- Ukatili huendelea kupitia ukimya, kukataa ukweli na kutokuchukua hatua.
- Manusura wameelezea matukio waliyoyapitia kwa ujasiri.
- Sasa uwajibikaji ni wetu sote.

MFUMO WA RUFAA KWA MANUSURA WA UKATILI WA KIJINSIA

MSAADA WA KISAIKOLOJIA & KIJAMII

- Nenda kwenye ofisi ya afisa ustawi wa jamii iliyopo karibu nawe kwa ajili ya mwongozo na rufaa.
- C-Sema (Kwa msaada wa watoto & rufaa) 24/7 ushauri nasihi + ufuatiliaji wa kesi.
- Mashirika yaliyojikita kwenye afya na Ukatili wa Kijinsia kwenye eneo lako.

MSAADA WA HARAKA

- **Dawati la Jinsia & Watoto la Polisi** (+255787668306) au ripoti kwa usalama katika kituo chochote cha polisi.
- Huduma za Kiafya: 199 (bure, 24/7, ushauri wa kitabibu na rufaa za dharura).

  Endapo unapitia ukatili wa kingono, hakikisha unapata huduma za kitabibu ndani ya masaa 72.

MSAADA 24/7

- C-Sema kwa Msaada wa Watoto: piga 116 (bure)

  Watoto, vijana, watu wazima, walezi, na jamii wanaweza kutoa ripoti na kupata taarifa.

  Unasihi katika hali ya usiri + Rufaa kwa huduma za kitaalamu.

HUDUMA ZA AFYA & KITABIBU

- Nenda hospital ya karibu au kituo cha mkono kwa mkono (One Stop Centre).
- Huduma zinahusisha:
  - Huduma za dharura (dawa kinga ya VVU (PrEP), matibabu, vipimo)
  - Msaada wa kisaikolojia-kijamii
  - Rufaa kwa ngazi za juu kwa vituo vya kutolea huduma za afya/ polisi/ huduma za kisheria

Endapo fomu #3 ya Polisi inapaswa kujazwa, sisitiza kipaumbele kwenye kupata huduma za kitabibu kwanza. Fomu inaweza kuletwa hospitali.

MFUMO PENDEKEZWA WA RUFAA
(sio kipimo kimoja kinachowatosha wote, kuripoti ni hiari)

Ongea na mtu unayemuamini/ piga simu namba za kutolea huduma | Pata huduma za matibabu (kwa haraka kama ni ukatili wa kingono) | Pata msaada wa kisheria + kisaikolojia-kijamii

HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA & HAKI

- **Wanawake katika Sheria na Maendeleo barani Afrika (WiLDAF)**

  0800 780 070 (namba ya bure)

  www.wildaftanzania.or.tz
- **Msaada wa kisheria + Mtandao wa Rufaa za Ukatili wa Kijinsia (Mkuki Coalition, Tanzania Legal Aid Providers Network – TANLAP)**

  +255 746 237 265
- **Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA)**

  0800751010 (namba ya bure) www.tawla.or.tz

  Dar es Salaam (na huduma katika mikoa mingine). Msaada wa kisheria, sapoti kwa kesi za ukatili wa kijinsia, uwakilishi.
- **Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC)**

  +255 22 215 3857 / +255 754 281 664 www.wlac.or.tz

  Dar es Salaam. Huduma za kisheria bure kwa wanawake na makundi yaliyo hatarini.
- **Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**

  +255 22 277 3038, /+255 754 300 345 www.humanrights.or.tz

  Dar es Salaam (huduma zinawafikia wananchi nchini kote). Huduma za kisheria, malalamiko kuhusu haki za binadamu, kesi za ukatili, uhamasishaji.

HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA & HAKI

- Nenda kwenye shirika la wasaidizi wa kisheria (paralegals) lililopo kwenye eneo yako kupata huduma za msaada wa kisheria bila malipo. Pia, watakusaidia na mifumo mingine ya rufaa.

MALAZI & CHAKULA

- Nenda kwenye ofisi ya afisa ustawi wa jamii iliyopo karibu nawe kwa mwongozo na rufaa
- Nenda ofisi ya karibu ya mtendaji wa kata au Kijiji kwa mwongozo na rufaa.
- Kama uko Dar es Salaam, Nyumba ya Amani; Msasani, +255 713 315 323, au Nyumba ya Watoto Kurasini

KUHUSU MRADI

Kitabu hiki ni matokeo ya mradi uliotekelezwa kuanzia Agosti 2025 hadi Juni 2026, uliolenga kuongeza uelewa wa umma kuhusu athari za ukatili wa kijinsia na kingono kwa manusura. Mradi ulitekelezwa na Women Action Towards Economic Development (WATED) kwa kushirikiana na programu ya Upatikanaji wa Haki kwa Kinamama na Watoto (SAFE) inayotekelezwa kwa pamoja na GIZ Tanzania na Wizara ya Katiba na Sheria.

Katika kipindi cha mradi, manusura 25 kutoka Dar es Salaam, Dodoma na Tanga walielezea hadithi ya matukio ya ukatili waliyokutana nayo na kupokea msaada wa kisaikolojia na kijamii. Hadithi hizi pia zinaoneshwa kupitia maonesho kwa njia ya cinema za kwenye gari katika mikoa hii mitatu pamoja na picha mjongeo (video).

SHUKRANI

Kitabu hiki kimewezekana kwa sababu ya ujasiri, imani na mshikamano wa pamoja.

Kwanza kabisa, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, idara husika za serikali, pamoja na mamlaka za serikali za mitaa za Tanga na Lushoto (Tanga), Bahi, Chamwino na Dodoma (Dodoma), na Temeke pamoja na Kinondoni (Dar es Salaam) kwa ushirikiano wao, msaada wao na ruhusa waliyoitoa katika utekelezaji wa mradi huu.

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa manusura waliochagua kushiriki hadithi zao. Sauti zenu zinabeba ukweli, maumivu, nguvu na heshima. Kitabu hiki kisingewezekana bila ujasiri wenu na imani yenu kwetu.

Tunatambua juhudi za watafiti na wawezeshaji wa kazi za uwanjani: Glory Mlaki na AnnaGrace Rwembuza waliokusanya ushuhuda kwa uangalifu, kulinda faragha ya manusura na kuhakikisha kila ushuhuda unaandikwa kwa heshima na utu.

Tunawashukuru pia timu ya uhariri na uwekaji kumbukumbu: Yvonne Guido (PRISEP), timu ya WATED, Wolflam Kiri, Hamisa Ally, Caroline Kochola na Columba Makono kwa kujitolea kuhifadhi sauti za manusura bila kubadilisha maana yake.

Shukrani kwa washauri wa huduma za kisaikolojia na kisheria, Grace Kipobota (HerGrace) na Angelina Mnyanyi (Beyond Wellness Centre), kwa kuhakikisha maadili, usalama wa manusura na mbinu zinazozingatia athari za kiwewe zinazingatiwa katika mchakato mzima.

Tunatoa pia pongezi kwa timu ya ubunifu na uzalishaji ya PREMIT Solutions Limited, Sengo Production na Debora Maboya kwa kuunda muundo unaoheshimu uzito wa hadithi hizi huku ukilinda heshima na utu wa wahusika.

Tunawashukuru washirika na wadau wetu - Fortunata Manyeresa, Tree of Hope Tanga, Miwhela Mapembe (ATIPWE Dodoma) na WAJIKI Dar es Salaam - kwa ushirikiano wao uliowezesha kazi hii.

Tunatoa shukrani za pekee kwa Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ), kupitia programu ya Access to Justice for Women and Children / Society in Action for Equality (SAFE), kwa msaada wa kiufundi na kifedha uliowezesha utekelezaji wa mradi huu. Tunathamini imani yao, mwongozo wao wa kitaalamu na ushirikiano wao katika kuendeleza upatikanaji wa haki, usawa na utetezi unaozingatia mahitaji ya jamii.

Tunatoa pia shukrani za dhati kwa Bodi ya Wakurugenzi ya WATED kwa mwongozo, ushauri na msaada wao usioyumba katika kuhakikisha utekelezaji wa kazi hii muhimu.

Mwisho, tunawatambua watu wote, mashirika na wanajamii wanaoamini kwamba ukimya si chaguo, na kusikiliza ni hatua ya kwanza kuelekea haki.

Kwa unyenyekevu na shukrani nyingi, tunawashukuru wote waliotembea nasi katika safari hii.

Maria Matui
Mkurugenzi Mtendaji, WATED.

VUNJA UKIMYA

VUNJA UKIMYA kinaunganisha sauti ambazo mara nyingi hunyamazishwa.
Kitabu hiki ni mkusanyiko wa shuhuda za
kweli kutoka kwa wanawake na wasichana Tanzania ambao wamepitia ukatili wa kijinsia na kingono.
Hizi si hadithi zinazosimuliwa kuhusu wao — ni hadithi wanazosimulia wao wenyewe,
kwa maneno yao, zikibeba maumivu, ustahimilivu na ujasiri.

Kuanzia unyanyasaji wa utotoni hadi ndoa za kulazimishwa,
kuanzia unyonyaji mashuleni na sehemu za kazi hadi ukatili uliofichwa ndani ya familia na mila,
sauti hizi zinaonyesha yale ambayo jamii mara nyingi huchagua kutoyaona.

Kitabu hiki kipo ili kusikiliza.
Kukumbuka.
Na kudai ukimya ukome.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

wafed

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by
giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH